HAKIARDHI

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE



TAARIFA YA MWAKA 2014

ISBN: 978-9987-626-27-4
Editorial: Cathbert Tomitho
Publisher: Land Rights Research and Resources Institute (LARRRI/HAKIARDHI)
Printed by: iPrint
Copyright: HAKIARDHI 2016

HAKIARDHI

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

TAARIFA YA MWAKA 2014

YALIYOMO

SURA YA KWANZA **4**

MUUNDO WA TAASISI YA HAKIARDHI 4

1. Utangulizi 4

2. Dira 4

3. Malengo/Madhumuni 4

4.0 Muundo wa Taasisi 5

4.1 Mkutano Mkuu wa wanachama. 5

4.2 Baraza la Ushauri 5

4.3 Bodi ya Wakurugenzi 5

4.4 Sekretarieti 5

5.0 Programu za Taasisi 6

5.1 Kitengo cha Utafiti, machapisho na utunzaji kumbukumbu 7

5.2 Kitengo cha Uhusishwaji jamii na Utetezi 7

5.3 Kitengo cha uendeshaji wa taasisi na usimamizi wa programu 7

6.0 Mafanikio 7

6.0 Changamoto 8

SURA YA PILI **10**

KITENGO CHA UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA TAARIFA 10

2. UTANGULIZI 10

2.1 UZALISHAJI WA TAARIFA KUPITIA TAFITI MBALIMBALI 10

2.1.1 Utafiti kuhusiana na Haki za Ardhi za Wananchi wanaoishi kwenye eneo la Hifadhi .

2.1.1 Matokeo ya utafiti yalikuwa kama ifuatavyo; 11

2.1.1.1Athari za matokeo ya migogoro katika jamii 12

2.1.1.1Mapendekezo; 13

2.2 Utafiti wa awali katika Wilaya za Kilolo na Mufindi, mkoani Iringa 13

2.2.1 Masuala yaliyoibuka ni pamoja na; 15

2.2.2 Mapendekezo ya Utafiti 19

2.3 Zoezi la kutambua mashirika na asasi za kiraia katika wilaya za programu 20

2.4 MACHAPISHO 21

2.4.1 Uzalishaji wa machapisho 21

2.4.2 Ununuzi wa Machapisho 21

2.5 UANDAAJI WA DOKUMENTARI 22

2.5.1 Dokumentari ya kongamano la kitaifa la masuala ya ardhi (NALAF) 22

2.6 USAMBAZAJI WA TAARIFA 22

2.6.1 Kusambaza Taarifa kupitia Tovuti 22

2.6.2 Usambazaji wa Taarifa kupitia Maktaba 24

2.6.3 Usambazaji wa Taarifa Kupitia Vyombo vya Habari 24

2.6.4 Usambazaji wa machapisho 29

SURA YA TATU 31

3.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KITENGO CHA UHUSISHWAJI JAMII 31

3.1 UTANGULIZI 31

3.2 PROGRAMU YA MAFUNZO YA HAKI ZA ARDHI NA UTAWALA VIJIJINI 31

3.3 UCHAMBUZI WA SHERIA ZA ARDHI NA MIJADALA NA WADAU KATIKA 38

3.3.1 Uchambuzi wa Rasimu ya Katiba na Baraza la Katiba la Taasisi 38

3.3.2 Uchambuzi wa Katiba pendekezwa 39

3.3.3 Msaada wa kisheria katika masuala ya ardhi 39

3.3.3.1 Wananchi waliopata usaidizi wa kisheria ofisini 39

3.3.3.2 Msaada wa kisheria katika wilaya za programu 40

3.4 USHIRIKI WA TAASISI NA JAMII JUU YA MASUALA YA ARDHI 41

3.4.1 Mijadala ya wazi katika wilaya za programu kuhusiana na haki za ardhi, utawala vijijini na mabadiliko ya tabianchi 41

3.4.1.1 Mijadala ya wazi katika wilaya za Kilolo na Mufindi 41

3.5 USHIRIKIANO NA TAASISI KITAIFA 44

3.5 KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA MTANDAO WA MASUALA YA ARDHI 49

3.5.1 Mijadala ya wabunge 49

3.6 UTEKELEZWAJI WA MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI VIJIJINI 50

3.6.1 Uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kijiji cha Magunguli na Wamimbalwe 50

3.6.2 Mpango wa matumizi ya ardhi kijiji cha Wambingeto na Lugalo wilaya ya Kilolo 51

3.6.3 Utoaji wa hatimiliki za kimila katika wilaya za Kilolo na Mufindi 51

SURA YA NNE 53

MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA HITIMISHO 53

Mafanikio ya jumla kutokana na utekelezaji wa kazi mbalimbali za taasisi 53

Changamoto za ujumla katika utekelezaji wa kazi za taasisi 54

HITIMISHO 54



SURA YA KWANZA

MUUNDO WA TAASISI YA HAKIARDHI

SURA YA KWANZA

MUUNDO WA TAASISI YA HAKIARDHI

1. Utangulizi

HAKIARDHI ni Taasisi ya kiraia iliyoundwa mwaka 1994 na kusajiliwa kama shirika lisilo la kiserikali, chini ya sheria ya Makampuni, Sura ya 212 ya Sheria za Tanzania. Taasisi ilianzishwa kwa kutambua umuhimu wa kuibua na kuendeleza mijadala juu ya umilikaji ardhi, kama mojawapo ya njia za kukuza ushiriki wa wananchi, hususan wazalishaji wadogo wadogo wa vijijini na pembezoni mwa miji, katika maamuzi yanayohusu ardhi na rasilimali nyingine muhimu zilizo katika maeneo yao.

2. Dira

Dira ya HAKIARDHI ni kuona kuwa raia wa Tanzania hususan wazalishaji wadogo wadogo wanakuwa na uhakika wa milki ya ardhi na rasilimali zao uliojengwa katika misingi ya usawa na haki katika kupata, kutumia, kumiliki na kudhibiti ardhi na rasilimali hizo kwa ajili ya maendeleo yao na ya taifa lao kwa ujumla.

3. Malengo/Madhumuni

Lengo kuu la HAKIARDHI ni kukuza ufahamu wa jamii juu ya masuala ya ardhi, kuimarisha mifumo ya utoaji wa maamuzi juu ya ardhi na kuwezesha ushiriki wa wananchi hususan wazalishaji wadogo wadogo waishio vijijini wanaokadiriwa kufikia 80% ya watanzania

wote, kwenye masuala ya ardhi ili waweze kudai, kutetea, kupata na kulinda haki zao za ardhi kwa manufaa yao. Malengo mengine ya Taasisi ni pamoja na:-

(i) Kutoa ushauri na misaada mingine ya aina hiyo kwa wazalishaji wadogo wadogo vijijini na kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji, kuhusu masuala ya kumiliki ardhi, na kutoa msaada wa kisheria katika kushughulikia baadhi ya mashauri ya ardhi kwenye vyombo vinavyohusika vya kisheria na kiutawala.

(ii) Kutoa huduma zitakazosaidia katika kutatua migogoro ya ardhi pale huduma hizo zitakapohitajika.

(iii) Kufanya utafiti juu ya masuala mbalimbali ya ardhi, kuunda na kupendekeza mbinu bora za kutatua migogoro ya ardhi kati ya vijiji na miongoni mwa wazalishaji wadogo wadogo.

(iv) Kuandaa na kuendesha kozi za muda mfupi kuhusu masuala ya milki na haki za ardhi Taasisi ikiombwa kufanya hivyo na makundi mbalimbali ya kijamii.

(v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali kama ushauri huo utahitajika na kama malengo yake yanahusiana na msimamo na mwelekeo wa Taasisi.

(vi) Kuandaa na kudhamini mikutano, semina na warsha na shughuli nyingine za namna hiyo kwa ajili ya kuendeleza malengo ya kijamii na kielimu ya Taasisi.

(vii) Kukusanya fedha za kuendesha shughuli za Taasisi bila ya kuathiri uhuru wa Taasisi wa kufanya kazi zake na malengo yake ya kielimu na kijamii.

4.0 Muundo wa Taasisi

Taasisi ya HAKIARDHI inaundwa na wanachama wenye hali na hadhi tofauti tofauti ambao hupatikana kutoka makundi mbalimbali ya kijamii. Uanachama uko wazi kwa mtu yeyote anayeamini, kujitoa na kujitolea katika kutetea haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo wadogo. Kiuendeshaji HAKIARDHI inaundwa na vyombo vikuu vinne ambavyo ni:-

4.1 Mkutano Mkuu wa wanachama.

Ni chombo kinachojumuisha wanachama wote na ndicho chombo cha juu kabisa ambacho kinatoa mwelekeo wa Taasisi. Mkutano Mkuu pia hupokea, hujadili na kupitisha mipango yote ya Taasisi, taarifa za fedha na utekelezaji pamoja na kuchagua Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi.

4.2 Baraza la Ushauri

Hushauri Bodi ya Wakurugenzi kuhusiana na masuala muhimu ya uendeshaji wa Taasisi.

4.3 Bodi ya Wakurugenzi

Hutoa muongozo wa kisera wa mipango ya Taasisi na kusimamia utekelezaji wake.

4.4 Sekretarieti

Inahusika katika kupanga na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Taasisi.

Muundo wa Taasisi



5.0 Programu za Taasisi

Katika jitihada za kufanikisha kufikia malengo ya Taasisi programu mbalimbali huandaliwa na kutekelezwa kulingana na fursa na uwezo wa kirasilimali wa Taasisi. Tangu mwaka 1994 hadi 2001, mipango ya Taasisi ilijikita katika kushawishi, kutetea na kuwezesha upatikanaji wa sera na sheria zinazozingatia matakwa na maslahi ya wazalishaji wadogo wadogo nchini. Sera ya taifa ya ardhi ya 1995 na sheria za ardhi za 1999 kwa kiasi kikubwa zilizingatia matakwa hayo japo baadhi ya masuala ya msingi yangali yakijadiliwa hasa kuhusiana na aina ya mfumo wa milki ya ardhi wenyewe.

Mwaka 2002 hadi 2006 HAKIARDHI ilitekeleza programu zinazohusu haki za ardhi kwa wachimbaji wadogo wadogo, athari za uporaji wa ardhi kwa wafugaji na wakulima wadogo wadogo na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mipango ambayo imekuwa ikitekelezwa tangu 2007 imejielekeza katika kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za masuala ya ardhi, elimu kwa umma, ushawishi na utetezi na kuimarisha vyombo vya utoaji maamuzi yanayohusu haki za wananchi kama vile mabaraza ya ardhi, halmashauri za vijiji na mikutano mikuu ya vijiji pamoja na kukuza ushiriki wa wananchi katika vyombo hivyo ili haki itendeke na ipatikane. Mipango hii hutekelezwa katika vitengo vitatu ambavyo ni:

5.1 Kitengo cha Utafiti, machapisho na utunzaji kumbukumbu

Lengo kuu la kitengo hiki ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na upatikanaji wa taarifa sahihi na za wakati kuhusiana na

masuala ya ardhi ili zitumike katika ushawishi na utetezi wa sera na sheria na pia katika kuandaa machapisho kwa ajili ya mafunzo ya ardhi vijijini na uelimishaji umma kwa ujumla. Shughuli kubwa ya kitengo hiki ni kufanya tafiti, kuhifadhi kumbukumbu na kuandaa machapisho mbalimbali kama vile vitabu, majarida, miongozo ya mafunzo. Matokeo ya tafiti husambazwa kwa wasomaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

5.2 Kitengo cha Uhusishwaji jamii na Utetezi

Lengo kuu la kitengo hiki ni kukuza uelewa wa wananchi juu ya mifumo ya umilikaji ardhi nchini na ushiriki wao kupitia vyombo vya usimamizi na maamuzi katika ardhi na rasilimali nyinginezo. Kitengo hiki huratibu shughuli zote za mafunzo ya uwezeshaji katika ngazi za vijiji hadi taifa, mafunzo ya sheria za ardhi, mijadala ya wazi, semina za kila mwezi za masuala ya ardhi, makongamano ya kitaifa na kimataifa, pamoja na utoaji wa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na ushiriki wa Taasisi katika shughuli za asasi nyingine.

5.3 Kitengo cha uendeshaji wa taasisi na usimamizi wa programu

Lengo kuu la kitengo ni kuhakikisha kunakuwepo na mfumo madhubuti katika uongozi na usimamizi wa rasilimali watu na fedha ili kufikia malengo ya Taasisi. Kitengo hiki kinahusika na vitengo vidogo vitatu ambavyo ni; (i) shughuli za uendeshaji wa kila siku wa taasisi (uratibu na usimamizi), (ii) utafutaji wa fedha, usimamizi wa fedha na ukaguzi wa mahesabu, (iii) ufuatiliaji wa shughuli zote za taasisi kulingana na miongozo na viwango vya ufanisi vilivyowekwa.

6.0 Mafanikio

(i) Utekelezaji wa mipango hiyo, umewezesha kufikiwa kwa watanzania takribani milioni kumi na tano na kukuza uelewa wao juu ya masuala ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini tangu Taasisi ilipoanzishwa. Maeneo hayo ni pamoja na vijiji zaidi ya 1,000 katika wilaya ambazo Taasisi imekuwa ikitekeleza programu zake kwa nyakati tofauti tofauti kama vile Mufindi, Kilolo, Newala, Rujewa, Kilwa, Kisarawe, Rufiji, Bagamoyo, Meatu, Kahama, Kiteto, Korogwe, Kilindi na Mkinga. Wilaya nyingine ni Kilosa, Kilombero, Mbarali, Morogoro vijijini, Ngorongoro, Hanang, Karatu, Kiteto na wilaya zote tatu za mkoa wa Dar es salaam yaani Temeke, Kinondoni na Ilala.

(ii) Taasisi imefanikiwa kuibua na kuendeleza mijadala juu ya haki za ardhi katika ngazi mbalimbali za kijamii ambayo imesaidia kuimarisha mifumo ya utoaji maamuzi, kupunguza na kuepusha migogoro ya ardhi na kuwezesha upatikanaji wa haki za ardhi na haki za binadamu katika maeneo husika.

(iii) Kadhalika, Taasisi imefanikiwa kufanya tafiti, kuandaa na kusambaza taarifa mbalimbali juu ya masuala ya ardhi (kama vile uwekezaji katika ardhi za vijiji na changamoto zake kwa jamii husika, rasilimali za baoanuai, mustakabali wa ufugaji na wafugaji nchini), na kusambaza kwenye jamii kwa kwa njia ya vitabu, majarida, vyombo vya habari na mijadala ya wazi ya kijamii.

(iv) Taasisi imekuwa ikishiriki katika michakato mbalimbali ya uandaaji wa sera na sheria kwa lengo la kutetea matakwa na maslahi ya wanyonge katika sheria hizo hususan sheria za ardhi na marekebisho yake mbalimbali.

(v) Kujenga nguvu za pamoja na washirika wengine wenye mlengo sawa na wa Taasisi kwa azma ya kuchangia jitihada za kuleta mabadiliko makubwa zaidi katika mfumo wa milki na matumizi ya ardhi ili kulinda haki na mstakabali wa wazalishaji wadogo nchini.

7.0 Changamoto

Mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini yametikisa mifumo ya kitaasisi na kijamii iliyokuwa ikisimamia maslahi ya moja kwa moja ya wananchi hususan wazalishaji wadogo wadogo. Katika mfumo wa sasa wa milki na matumizi ya ardhi ambao umeigeuza ardhi kuwa bidhaa ya kushindaniwa, ni dhahiri kwamba maslahi ya wazalishaji wadogo yanapaswa kuangaliwa zaidi kwa vile nguvu yao ya kushindana katika soko ni ndogo kulinganisha na makundi mengine yenye uwezo kiuchumi, kisiasa na kijamii. HAKIARDHI na asasi za aina yake zina wajibu wa kuendelea kupigania, kulinda na kutetea maslahi hayo katika sera na sheria na mifumo ya usimamizi wa haki za ardhi katika jamii.

Uhaba wa rasilimali bado ni changamoto kubwa kwani Taasisi hushindwa kufanya kazi katika maeneo makubwa zaidi. Bila shaka, upatikanaji wa rasilimali fedha zaidi utawezesha kuwa na rasilimali watu zaidi na vitendea kazi zaidi na hivyo kuwezesha Taasisi kuwafikia watu wengi zaidi katika ngazi ya jamii.

Migogoro ya ardhi kati ya makundi mbalimbali ya kijamii bado inaendelea na athari zake zimezidi kuwa kubwa hasa kutokana na upotevu wa mali na maisha ya wananchi wasio na hatia wakiwemo wanawake, watoto na wazee. Serikali, asasi za kiraia na washirika wengine hawana budi kuendelea kuimarisha mifumo ya kiasili na ile rasmi ya utatuzi wa migogoro ili kuepusha athari zaidi kwa wananchi.

SURA YA PILI

KITENGO CHA UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA TAARIFA

SURA YA PILI

KITENGO CHA UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA TAARIFA

2. UTANGULIZI

Kitengo cha Uzalishaji na Usambazaji wa taarifa kimegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni (i) Uzalishaji wa taarifa, na (ii) Usambazaji wa taarifa. Uzalishaji wa taarifa hufanywa kupitia tafiti, utafiti mdogo wa kutafuta ukweli, na uchambuzi wa sera na sheria za masuala ya ardhi na rasilimali. Usambazaji wa taarifa hizo hufanyika kupitia tovuti, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, maktaba na vipindi katika vyombo vya habari kwa maana ya televisheni na radio. Kwa ujumla kitengo hiki huwezesha kitengo cha Uhusishwaji Jamii katika kutekeleza kazi zake kupitia ushawishi na utetezi wa haki za ardhi za wazalishaji wadogowadogo ambao ni wakulima, wafugaji, wachimba madini wadogo na waokota matunda. Taarifa hizi pia ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa mafunzo ya haki za ardhi na utawala katika wilaya za programu.

2.1 UZALISHAJI WA TAARIFA KUPITIA TAFITI MBALIMBALI

Uzalishaji wa taarifa kupitia tafiti ndio nguzo kuu ya kuanzishwa kwa Taasisi ya HAKIARDHI yenye lengo kuu linalosema “Kukuza utafiti kwenye haki za ardhi za wazalishaji wadogo wadogo ambao ni pamoja na wakulima na wafugaji kwa lengo la kutoa taarifa na maarifa ili kuwezesha kupatikana kwa mfumo wa haki na usawa katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na mahitaji mengine.” Katika kuhakikisha kuwa sera na sheria za ardhi zinafanyiwa

mabadiliko makubwa mchakato mzima unatakiwa kuwa na taarifa sahihi na za wakati. Kitengo cha utafiti kimegawanywa katika sehemu kuu tatu ambazo ni;

Tafiti kubwa ni zile tafiti za kimkakati ambazo zimelenga kuzalisha taarifa za kutumika kwenye masuala ya utetezi kwa watunga sera, sheria, wafanya maamuzi na kwajili ya umma kwa ujumla wake. Wakati tafiti za awali kwenye wilaya za kiprogramu ni mahususi kwajili utekelezaji wa programu ya mafunzo ya haki za ardhi na utawala vijijini. Tafiti ndogo za utafutaji ukweli na majibu ya haraka ni zile tafiti zinazohusiana na ufuatiliaji wa masuala ya dharura yanayoibuka kama vile migogoro ya ardhi, uwekezaji na uporaji wa ardhi, lengo likiwa ni kupata taarifa sahihi kwaajili ya utetezi na ushawishi wa haki za ardhi za wazalishaji wadogowadogo.

Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na taarifa za kutosha katika kipindi cha mwaka 2014 kitengo hiki kilitekeza kazi zifuatazo;

2.1.1 Utafiti kuhusiana na Haki za Ardhi za Wananchi wanaoishi kwenye eneo la Hifadhi ya Taifa ya Saadani.

Mgogoro baina ya wanakijiji wa kitongoji cha Uvinje, kijiji cha Saadani wilayani Bagamoyo ambao umedumu kwa muda mrefu na kuathiri haki za ardhi za wananchi hawa katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi kwenye maeneo yao ya asili. Kutokana na kukithiri kwa malalamiko ya kukiukwa haki za ardhi za wananchi hawa Taasisi ya HAKIARDHI iliamua

kufanya utafiti hapo tarehe 8 – 14 Aprili 2014 kwa lengo la kupata ukweli kuhusiana na mgogoro husika hasa kuhusiana na vyanzo, athari na hatua za utatuzi wa mgogoro husika zilizochukuliwa na mamlaka mbalimbali katika nyakati tofauti.

Picha 1: Eneo la fukwe katika kitongoji cha Uvinje, kijiji cha Saadani

2.1.1 Matokeo ya utafiti yalikuwa kama ifuatavyo;

- Mamlaka zinazojihusisha na kuunda hifadhi za wanyama pori hazikutumia mbinu shirikishi katika kuitangaza mbuga ya Saadani kuwa mbuga ya hifadhi. Mbinu shirikishi hazikutumika katika mchakato wa kuianzisha Saadani National Park kwani wananchi hawakupewa taarifa sahihi katika hatua za awali badala yake walishirikishwa katika hatua za mwisho. Hakukuwa na mashauriano yoyote

miongoni mwa wananchi na viongozi wao juu ya nia ya serikali kubadili hifadhi kutoka Game Reserve kwenda kuwa Hifadhi ya Taifa (National Park).

- Mgogoro huu umefikia hatua mbaya kutokana na serikali kupuuza malalamiko na mahitaji ya wanakijiji. Viongozi kadhaa wa kisiasa na watendaji wa serikali wamejulishwa juu ya mgogoro huu pasipo kuchukua hatua yoyote madhubuti bali huishia kutoa ahadi zisizotekelezwa.
- Sababu ya zinazopelekea wanakijiji kutokuwa na utayari wa kukubali fidia kutoka Hifadhi ya Taifa ni kutokana na ukweli kwamba maoni yao yalikuwa yamepuuzwa juu ya mchakato mzima wa kuanzisha Hifadhi ya taifa. Pia fidia iliyopendekezwa kulipwa haikuwa fidia sahihi kwasababu kanuni za ulipwaji fidia zinataka fidia iwe ni kamili ya haraka na wakati. Mchakato wa uthamini mali uliofanywa na serikali haukutilia maanani muda na nguvu wananchi waliyotumia katika kuliendeleza eneo hilo kabla ya kufanywa Hifadhi. Moja ya madai ya wananchi ni kuwa walipwe fidia ya kuliendeleza eneo hilo la fukwe katika kipindi chote walichoishi hapo.
- Utatuzi wa mgogoro huu umegeuzwa mtaji wa kisiasa kwa wanasiasa kuutumia katika kufanikisha malengo yao ya kisiasa ikiwa ni pamoja na kupata kura za kuwawezesha kuwa madiwani na wabunge. Ilibainika kwamba viongozi mbalimbali wa kisiasa kama vile Madiwani, Wabunge, Wakuu wa Wilaya, Mkoa na viongozi wa vyama vya siasa hutembelea eneo hilo mara kadhaa na kuishia katika kutoa hotuba za kisiasa ambazo kamwe hazileti usuluhishi juu ya mgogoro.

2.1.1.1 Athari za matokeo ya migogoro katika jamii

- Mgogoro huu umesababisha wananchi kutokunufaika na fukwe ya bahari ya pwani kwa uwekezaji kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa kwa sababu sasa watalii wanapaswa kutoa taarifa na kulipa ada ya kiingilio kwenye uongozi wa TANAPA.
- Wanakijiji hawajihusishi tena na shughuli za kijamii na kiuchumi kwa sababu mamlaka ya Hifadhi ya Taifa inatumia nguvu kubwa kuwazuia ikiwa ni pamoja na kutumia askari wenye silaha za moto. Kwa mfano wanakijiji wamezuiwa kujenga majengo ya shule ya msingi.
- Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Taifa haitoi ulinzi wa maisha na mali za wanakijiji juu ya wanyama pori hatari.

2.1.1.1 Mapendekezo;

- Asasi za kiraia zinazojishughulisha na haki za ardhi hususan TALA kuongoza jopo la utetezi wa haki za ardhi za wananchi wa eneo hili ikiwa ni pamoja na kuishinikiza serikali kutenga upya eneo hilo na kuzingatia haki za wanakijiji katika ardhi.
- Kufanya mafunzo ya haki za ardhi na utawala kwa wanakijiji na viongozi ili kuongeza uwezo wao wa utambuzi wa haki za ardhi, pia kufahamu njia na mbinu stahiki kwa mujibu wa sheria katika kuitafuta haki yao.
- Kusaidia wanakijiji kufungua kesi katika Mahakama Kuu na kuomba hatua za kisheria zichukuliwe juu ya suala hilo.

2.2 Utafiti wa awali katika Wilaya za Kilolo na Mufindi, mkoani Iringa

Wilaya za Kilolo na Mufindi zilizopo mkoani Iringa ni wilaya zilizochaguliwa kuwa wilaya za kiprogramu kwa Taasisi kwa mwaka 2014. Ili kuanza utekelezaji wa programu katika wilaya hizi ni lazima kufanya utafiti wa awali kwa lengo la kutambua mahitaji ya kiprogramu pamoja na kuitambulisha programu kwa viongozi wa wilaya, vijiji na wananchi wa vijiji husika.

Utafiti huu ulitekelezwa kati tarehe 21 Julai - 5 Agosti 2014 katika wilaya hizi mbili ambapo pamoja na kukusanya taarifa za masuala ya ardhi pia kulibainishwa vijiji ambavyo programu itatekelezwa kwa kipindi chote. Vilevile utafiti ulilenga kukusanya taarifa juu ya masuala ambayo ni changamoto katika usimamizi na matumizi ya ardhi, matatizo ya utawala katika vyombo vya kijiji ikiwa ni pamoja na kusimamia na kufanya maamuzi sahihi, aina ya migogoro juu ya matumizi ya ardhi pamoja na masuala mengine kama vile haki za wanawake katika ardhi, mabadiliko ya tabia nchi na uwekezaji katika ardhi ya kijiji.

Picha 2: Sehemu ya wanakijiji waliohudhuria mahojiano utafiti katika kijiji cha Idasi, Kilolo

Matokeo yalikuwa;

Vijiji vilivyochaguliwa kwa ajili ya programu vilikuwa ni;

NO	WILAYA	VIJIJI	NO	WILAYA	VIJIJI
	KILOLO			MUFINDI	
1	"	Ilutila	1	"	Ihomasa
2	"	Madege	2	"	Kasanga
3	"	Idasi	3	"	Nyigo
4	"	Masisiwe	4	"	Kinegembasi
5	"	Nyawegete	5	"	Tambalang'ombe
6	"	Ng'ingula	6	"	Kibada
7	"	Lugalo	7	"	Kipanga
8	"	Uhambingeto	8	"	Ilogombe
9	"	Kitumbuka	9	"	Nyakipambo
10	"	Ikuka	10	"	Ipilimo

Chanzo: Utafiti wa awali 2014

2.2.2 Masuala yaliyoibuka ni pamoja na;

(i) Mamlaka ya Halmashauri ya Kijiji

Ilibainika kuwa wajumbe wa halmashauri za kijiji hawatambui majukumu/mamlaka ya Halmashauri ya Kijiji katika kusimamia ardhi ya kijiji. Baadhi ya wajumbe wana dhana kuwa ni viongozi wa juu katika serikali ndio wenye mamlaka ya kuamua juu ya masuala yanayohusiana na ardhi ya kijiji.

Vilevile maamuzi yanayotolewa na viongozi wa serikali ngazi ya wilaya na serikali kuu wakati mwingine hayafuati kanuni za Sheria za Ardhi hivyo kuwapa wakati mgumu viongozi wa halmashauri za vijiji katika utekelezaji wake na kuwa

chanzo cha kuhitilafiana na wananchi wanaowaongoza. Tafsiri ya maelekezo haya ni kuwa hakuna ushikishwaji madhubuti wa wananchi katika masuala yanayohitaji maamuzi yao juu ya ardhi ya kijiji.

Kwa mfano katika baadhi ya vijiji katika wilaya hizi, Wakuu wa Wilaya na Madiwani wamekuwa wakiingilia mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Bahati mbaya maamuzi ambayo wamekuwa wakiyafanya yamekuwa chachu ya kuongeza migogoro zaidi kutokana na viongozi hawa kutoa maamuzi ambayo kwa undani wake yanakuwa na upendeleo kwa kundi moja kati ya makundi yenye mgogoro.

(ii) Mamlaka ya Mkutano Mkuu wa Kijiji

Utafiti ulibainisha kuwa Mikutano Mikuu ya Vijiji imekuwa ikiendeweshwa kimakosa kutokana na viongozi wa vijiji kutokukufahamu au kutokuijua vyema sheria inayosimamia masuala ya utawala kwenye Serikali za Mitaa nchini ambayo ni Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sheria ya 1982. Viongozi wengi hasa Wenyeviti wa vijiji wana uelewa mdogo juu ya mamlaka na wajibu wa Mkutano Mkuu katika kufanya maamuzi yanayohusu kijiji. Pia kutokana Mikutano Mikuu kuendeshwa pasipo kufuata taratibu za kisheria kumetoa mwanya ya mambo makubwa ya ardhi kuamuliwa na wanakijiji wachache na viongozi ambao sio wawakilishi wa watu wengi katika kijiji.

Kwa mfano mamlaka ya Mkutano Mkuu katika kupitisha wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji imefanywa kuwa ni wajibu wa halmashauri ya kijiji.

Picha 3: Baadhi ya wananchi waliohudhurio Mkutano Mkuu kijijini Kidabaga, Kilolo

(iii) Kamati ya Maamuzi ya Kijiji

Utafiti ulibaini katika vijiji vilivyochaguliwa kwa ajili ya mradi hakuna kijiji kilichounda kamati hii badala yake majukumu ya kamati hii yanatekelezwa na kamati nyinginezo kama vile Kamati ya Huduma za Jamii au Mwenyekiti na Mtendaji wa Kijiji.

(iv) Hali ya Utekelezaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika Wilaya

Ilibainika kuwa uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ni wa kusuasua sana katika wilaya hizi hasa utekelezaji unaofanywa na Halmashauri za Wilaya husika. Ni vijiji vichache vilivyobainishwa kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi. Pia kilichobainika ni kuwa kuna baadhi ya vijiji ambavyo kumbukumbu zinaonyesha kuwa mpango wa matumizi ya ardhi umeshaandaliwa lakini katika hali halisi mpango huo haulingani na taratibu za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Mpango Matumizi ya Ardhi ya 2007. Kwa mfano karibu vijiji vyote ambayo vilitaja kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi havikuwa na Cheti cha Ardhi ya Kijiji na hakuna mwanakijiji yeyote aliyepatiwa Cheti cha hatimiliki ya Kimila.

(v) Soko la Ardhi katika Wilaya

Ilibainishwa kwamba soko la ardhi katika wilaya za Kilolo na Mufindi linakua kwa kasi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahitaji ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika mashamba ya miti kwa ajili ya biashara ya mbao. Utafiti ulibaini bei mbalimbali kati ya shilingi 100,000 / = adi 1,000,000 / = kwa ekari. Soko la upatikanaji wa kuuza ardhi unafanywa na viongozi wa vijiji hasa Maafisa Watendaji wa vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji. Watendaji hawa huandaa mikataba ili kuweza kuidhinisha uhamishaji wa miliki ya ardhi (manunuzi).

Hali ya migogoro ya ardhi katika wilaya za Kilolo na Mufindi

NO	MIGOGORO YA ARDHI	SABABU ZA MIGOGORO YA ARDHI	VIJIJI
1	Migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji	Kuongeza kwa mifugo katika vijiji, Mahitaji makubwa ya ardhi kwa ajili ya kilimo uitaji wa ardhi kwa Wawekezaji kwa ajili ya uwekezaji	Uhambingeto, Kitumbuka, Ikuka and Nyigo.
2	Migogoro ya mipaka baina ya vijiji	Ukosefu wa mpango wa matumizi ya ardhi kijijini ushirikishwaji hafifu kwa wanakijiji katika upimaji wa ardhi usimamizi mbovu wa ardhi ya kijiji ongezeko la Idadi ya Watu	Uhambingeto, Kitumbuka, Ikuka, Nyigo, Lugalo
3	Migogoro baina ya wakulima na wakulima	Ongezeko la thamani ya ardhi Kupanda kwa soko la ardhi Athari mabadiliko ya tabia nchi	Vijiji vyote vimeathirika

Chanzo: Utafiti wa awali 2014

Hali ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji Wilaya ya Mufindi

No	Kijiji	Wajumbe	Hali halisi	Mwaka wa kuanzishwa	Taratibu (Malipo ya kufungua kesi na kutembelea eneo)
1	Ihomasa	Hakuna wajumbe	Baraza halijaundwa	-	-
2	Kasanga	Hakuna wajumbe	Baraza halijaundwa	-	-
3	Nyigo	8(4 ke)	Baraza limeundwa	1996	15,000/=(kufungua kesi); 20,000/=(kutembelea eneo)
4	Kinegembasi	9(2 ke)	Baraza limeundwa	2007	Hamna taarifa
5	Tambalang'ombe	8(4 ke)	Baraza limeundwa	2010	2,500/= (kufungua kesi); 20,000/= (kutembelea eneo)
6	Kibada	hakuna wajumbe	Baraza halijaundwa		-
7	Ilogombe	7 (4 ke)	Baraza lipo halifanyi kazi	2010	-
8	Kipanga	8(4 ke)	Baraza lipo halifanyikazi	2007	-
9	Ipilimo	6(3 ke)	Baraza limeundwa	2011	3,000/=(kufungua kesi); 120,000/=(kutembelea eneo)
10	Nyakipambo	7(3 ke)	Baraza lipo halifanyi kazi	2011	Hamna taarifa

Chanzo: Utafiti wa awali 2014

Hali ya Mabaraza ya Kata

No	Ngazi ya Kata Mufindi	Wajumbe	Mwaka kuanzisha	Taratibu (Malipo ya ufunguzi kesi na kutembelea eneo la migogoro)
1	Idete	7(0 ke)	2011	Hakuna taarifa
2	Nang'ang'e	8(4 ke)	2013	20,000/= (kufungua kesi); 80,000/= (kutembelea eneo)
4	Bomalang'ombe	8(3 ke)	2013	13,500/= (kufungua kesi); 70,000/= (kutembelea eneo)
5	Ilole	8(3 ke)	2014	12,000/= (kufungua kesi); 80,000-100,000/=(kutembelea eneo)
No	**Ngazi ya Kata Mufindi**	**Wajumbe**	**Mwaka kuanzisha**	**Taratibu (Malipo ya ufunguzi kesi na kutembelea eneo la migogoro)**
1	Itandula	11(6ke)	2014	10,000/= (kufungua kesi); 100,000/= (kutembelea eneo)
2	Kibengu	7(3 ke)	2013	45,000/= (kufungua kesi); 200,000/= (kutembelea eneo)
3	Mtambula	6(3 ke)		10,000/= (kufungua kesi); 140,000/= (kutembelea eneo)
4	Sadani	7(3 ke)	2010	5,000/= (kufungua kesi); 40,000- 50,000/= (kutembelea eneo)

Chanzo: Utafiti wa awali 2014

Changamoto zinazovikabili vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi Kilolo na Mufindi

No	Tatizo	Mapendekezo
1.	Ukosefu wa mafunzo kwa wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya vijiji na mabaraza ya kata juu ya masuala ya ardhi	Wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya vijiji na mabaraza ya kata wanapaswa kupatiwa mafunzo juu ya masuala ya ardhi mara tu wanapoteuliwa
2.	Ushirikishwaji hafifu kwa wanawake katika kufanya maamuzi.	Wanawake washirikishwe katika mchakato wa utoaji wa maamuzi.
3.	Kuingiliwa kwa maamuzi ya baraza la kijiji na viongozi wa kisiasa katika migogoro ya ardhi.	Viongozi wa vijiji na wanasiasa wanapaswa kupewa taarifa juu ya ukomo wao katika ardhi ya kijiji.
4.	Ukosefu wa elimu miongoni mwa wanakijiji juu ya sheria za ardhi	Wanakijiji lazima wapatiwe mafunzo ya haki za ardhi na utawala.
5.	Gharama zinazotumika na Baraza la Ardhi la Kijiji na Baraza la kata ni ghali kwa wanakijiji walio wengi.	Vyombo hivi lazima vitenge gharama itakayoweza kugaramikiwa na wanakijiji wengi.

Chanzo: Utafiti wa awali 2014

2.2.3 Mapendekezo ya Utafiti

- Kuwajengea uwezo wa sheria za ardhi wajumbe wa vyombo vya utawala kijijini kuhusu majukumu yawapasayo katika kusimamia ardhi ya kijiji kama njia ya kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo ya vijijini.
- Kusaidia vijiji kuelewa taratibu na mchakato wa uwekezaji katika ardhi ya kijiji ili kuwawezesha kushiriki vizuri katika mchakato na kuepukana madhara ya muda mrefu ambayo ni pamoja na migogoro ya ardhi.

- Halmashauri za wilaya zifanye usimamizi na ukaguzi wa ugawaji wa ardhi vijijini ili kubaini nani ni mmiliki wa eneo gani kama njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya ardhi siku za baadaye. Jambo hili linapaswa kwenda sambamba na kuchunguza kama taratibu za ugawaji ardhi zilizingatiwa.
- Ushirikishishwaji uliomkamilifu katika kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji ni chaguo bora kwa ajili ya kutambua haki za wazalishaji wadogo katika ardhi kwa maana inasaidia jamii kupanga juu ya matumizi ya ardhi yao. Mpango wa matumizi ya ardhi husaidia wanakijiji kupanga na kukubaliana juu ya matumizi bora ya ardhi yao.
- Asasi za kiraia kupitia TALA waandae mijadala ya wazi kwa umma juu ya haki za ardhi hususan katika ngazi ya kijiji ili kuwawezesha wanakijiji na viongozi wao kuelewa wajibu wao na majukumu katika kulinda ardhi ya kijiji.

2.3 Zoezi la kutambua mashirika na asasi za kiraia katika wilaya za programu

Utetezi wa haki za ardhi kwa wazalishaji wadogowadogo sio jukumu linaloweza kufanywa na shirika moja au mashirika machache bila ya kuwa na muunganiko wa pamoja na mashirika mbalimbali kwa lengo la kutetea haki za wazalishaji wadogowadogo. Hapa nchini Tanzania mipango hiyo ilikwishaanza kwa kuanzishwa Mtandao wa Asasi zinazojihusisha na utetezi wa haki mbalimbali kwa wananchi, mtandao huu unafahamika kwa jina la Tanzania Land Alliance (TALA).

HAKIARDHI imeendelea na mipango ya kuhakikisha kwamba asasi za kiraia zinazojihushisha na utetezi wa haki za binadamu, haki za ardhi, kijamii na harakati za kimazingira zinaungana kwa manufaa ya wazalishaji wadogowadogo. Katika kipindi cha mwaka 2014 Taasisi ilifanya utafiti wa kubainisha mashirika ya kijamii katika wilaya za Kilolo na Mufindi, mkoani Iringa. Madhumuni ya kubainisha mashirika na asasi hizi ni kuiwezesha HAKIARDHI kuwajengea uwezo katika ufanyaji wa wa utetezi na ushawishi wa haki za ardhi, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi kwa wafanyakazi na wanachama wa mashirika husika.

Katika utafiti huu taasisi zilizobainishwa ni 47 ambazo ni taasisi zisizo za kiserikali (NGO's) katika ngazi ya wilaya, taasisi 26 zinazojihusisha na masuala ya kijamii kama vile afya na magonjwa na taasisi 28 za kijamii zinazojihusisha na masuala ya mazingira, misitu na kilimo. Ilibanika kuwa baadhi ya taasisi hizi zilihitaji kujengewa uwezo katika masuala mbalimbali ila maeneo ya muhimu kwa wakati huu ni mawili ambayo ni. Moja ni utekelezaji na usimamizi wa fedha hasa katika kutafuta fedha na usimamizi na utunzaji sahihi wa kumbukumbu. Mbili mengi ya taasisi zilizobainishwa hazikuwa na kipengele cha utetezi wa haki za ardhi katika programu zao na miradi pamoja na kwamba kila shughuli wanazo zifanya vijijini zina mahusiano ya moja kwa moja na rasilimali ardhi kwa mfano wale wanaofanya kazi katika maeneo ya misitu na usimamizi wa mazingira.

2.4 MACHAPISHO

2.4.4 Uzalishaji wa machapisho

Katika kipindi cha mwaka 2014, HAKIARDHI ililenga kuzalisha machapisho mbalimbali kwa madhumuni ya kutumiwa na wafanyakazi kuongeza ufanisi katika kazi utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile machapisho haya huandaliwa kwa lengo la kwawezesha wasomaji wengine kujifunza masuala ya ardhi. Machapisho yaliyozalishwa kwa madhumuni ya kujifunza yalikuwa na lengo la kuwawezesha wananchi juu ya masuala yanayohusu haki za ardhi, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi wakati kwa upande mwingine machapisho kwa ajili ya utetezi wa sera na sheria za mapitio na matokeo ya utafiti, utafiti wa kutafuta ukweli na uchambuzi wa sera. Machapisho hayo ni pamoja na vijarida vya kujielimisha, majarida "Ardhi ni Uhai", vipeperushi, kalenda za mwaka, na miongozo ya mafunzo. Kwa kipindi cha mwaka mzima Taasisi imeweza kuzalisha nakala 33,500 za machapisho mbalimbali kutokana na kazi zake. Idadi ya nakala za machapisho haya yamekuwa yakisambazwa kwa wadau mbalimbali.

2.4.5 Ununuzi wa Machapisho

HAKIARDHI imekuwa ikinunua machapisho mbali mbali kutegemeana na mahitaji ya watumishi na maktaba ya taasisi. Jumla ya machapisho 266 yenye mada mbalimbali juu ya haki za ardhi, masuala ya maendeleo, usimamizi wa rasilimali, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Machapisho haya hununuliwa kulingana na mombi kutoka kwa wafanyakazi na wasomaji ambao hutembelea maktaba ya taasisi.

2.5 UANDAAJI WA DOKUMENTARI

2.5.1 Dokumentari ya kongamano la kitaifa la masuala ya ardhi (NALAF)

Kongamano la kitaifa la masuala ya ardhi kwa mwaka 2014 liliambatana na maadhimisho ya miaka 20 ya kuanzishwa kwa Taasisi ya HAKIARDHI. Mada mbalimbali ziliandaliwa na kuwasilishwa na washiriki kutoka katika taasisi kadhaa na kuibua mjadala mkubwa miongoni mwa washiriki zaidi ya 100 walioshiriki kongamano hilo. Kutokana na umuhimu wa kongamano na mada zilizojadiliwa Taasisi iliandaa dokumnetari kwa lengo la kuhkikisha kuwa jamii nzima ya Watanzania wanapata kusikiliza mjadala huo kupitia vyombo vya habari. Dokumentari hii iliandaliwa na kurushwa kupitia kituo cha televisheni cha TBC1 hapo mwezi Novemba na Desemba 2014.

2.6 USAMBAZAJI WA TAARIFA

LENGO MKAKATI 2: - Kuongezeka Kwa upatikanaji wa Taarifa za Kuaminika na Sahii Juu ya Masuala ya Ardhi.

2.6.1 Kusambaza Taarifa kupitia Tovuti

HAKIARDHI inatumia tovuti katika usambazaji wa taarifa za ardhi, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Katika mwaka 2014 Taasisi iliendesha tovuti mbili ambazo ni www.hakiardhi.org na www.tabef.org, tovuti hizi kwa pamoja zinatumika kama sehemu ya kupashana taarifa mbalimbali za ardhi zinazokusanywa na kuchambuliwa kiumakini na kurushwa humo kwa lengo la watu kujisomea. Tovuti hizi kwa mwaka

2014 zilivutia watu wengi kutambua kazi zinazofanywa na Taasisi pamoja na ubora wa kazi na mafanikio ya kazi husika kwa malengo ya kusaidia wazalishaji wadogowadogo nchini. Wasomaji wakubwa wa taarifa za kimtandao katika tovuti za Taasisi ni wanafunzi wa vyuo vikuu nchini na nje ya nchi, watafiti wa masuala ya ardhi, mazingira, misitu na madini pamoja na wafanyakazi wa taasisi mbalimba za serikali na binafsi.



Picha 4: Kurasa ya mbele ya tovuti ya www.hakiardhi.org

HAKIARDHI
Jumla wageni waliofungua tovuti HAKIARDHI kutoka Januari – Desemba 2014. Chanzo www.hakiardhi.org

Mwezi	Wageni	Idadi ya waliotembelea	Idadi ya Pakua
Jan 2014	2,720	7,690	69,780
Feb 2014	3,880	8,450	89,570
Mar 2014	4,350	7,790	103,790
April 2014	3,610	8,310	98,850
May 2014	2,620	4,919	49,061
Jun 2014	2,430	4,817	39,419
Jul 2014	2,448	5,558	73,015
Aug 2014	2,328	5,056	138,113
Sep 2014	1,272	2,470	74,255
Oct 2014	2,841	6,109	184,384
Nov 2014	3,359	6,229	180,433
Dec 2014	5,485	8,240	152,447
Jumla	**48,798**	**75,638**	**1,253,117**

TABEF
Jumla wageni waofungua tovuti TABEF kutoka Januari – Desemba 2014. Chanzo www.tabef.org

Mwezi	Wageni	Idadi ya waliotembelea	Idadi ya Pakua
Jan 2014	173	241	3,789
Feb 2014	201	380	2,760
Mar 2014	194	240	1,420
April 2014	261	427	2,460
May 2014	214	376	3,136
Jun 2014	237	404	2,274
Jul 2014	195	298	1,142
Aug 2014	162	257	1,733
Sep 2014	84	121	823
Oct 2014	127	207	1,584
Nov 2014	48	72	787
Dec 2014	56	69	820
Jumla	**1,952**	**3,092**	**22,728**

2.6.2 Usambazaji wa Taarifa kupitia Maktaba

Maktaba ya HAKIRDHI ni sehemu muhimu ambayo inatumika kuhifadhi machapisho mbalimbali yanayoalishwa na Taasisi yenyewe na yale yanayonunuliwa kutoka katika taasisi nyingine. Lengo kuu la kuwa na maktaba ni kutoa fursa kwa wananchi wa kada mbalimbali pamoja na wageni wa nje ya nchi kufika na kujisomea masuala ya ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa yanapatikana katika taasisi ya HAKIARDHI ukilinganisha na taasisi nyinginezo za binafsi au za umma. Kwa mwaka 2014 jumla ya wasomaji 53 (17 wanawake) walifika katika maktaba kwa lengo la kujisomea machapisho ya masuala ya ardhi, mazingira, misitu pamoja na sheria mbalimbali zinazosimamia rasilimali husika.

2.6.3 Usambazaji wa Taarifa Kupitia Vyombo vya Habari

HAKIARDHI imekuwa kwa muda mrefu ikitumia vyombo vya habari katika kusambaza taarifa zake kwa jamii. Kwa mwaka 2014 Taasisi iliendelea kutumia vyombo vya habari kama mkakati wa kufikia umma ndani na nje ya maeneo ya programu zake. Matumizi ya vyombo vya habari yameonesha kuwa chanya kwa kuwa na ongezeko la watu ambao hutembelea ofisi za Taasisi wakitafuta ushauri wa kisheria baada ya kupata mafunzo kupitia vyombo vya habari. Pia kuna ongezeko la wasomaji wa machapisho ambao wamehamasishwa kutokana na kusikiliza katika radio au kuona katika runinga na kusoma magazeti. HAKIARDHI inafikia vyombo vya habari kwa njia mbili moja ni kupitia vipindi ambavyo Taasisi inavilipia yenyewe na pili ni kupitia vipindi vya bure vya kuelimisha jamii vinavyotolewa na redio husika.

Utekelezaji wa vipindi vya redio kwa mwaka 2014 katika jedwali hapa chini;

Vipindi vya Radio vilivyorushwa hewani vilikuwa;

Kituo cha Radio	Mada	Aina ya kipindi	Washiriki	Tarehe ya urushwaji
Furaha FM	Historia ya umiliki wa ardhi nchini Tanzania kupitia.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	14/07/2014
Furaha FM	Vyombo vya usuluhishi wa migogoro wa ardhi na majukumu yao katika kutatua migogoro ya ardhi.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	15/07/2014
Furaha FM	Masuala muhimu ya kuzingatiwa na wananchi katika ardhi ya kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	16/07/2014
Furaha FM	Mabadiliko ya tabia nchi na haki za ardhi za wazalishaji wadogowadogo.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	17/07/2014
Furaha FM	Vyombo vya utawala kijijini na majukumu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	18/07/2014
Furaha FM	Athari za mabadiliko ya tabia nchi kwenye haki za ardhi kwa wanawake.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	21/07/2014
Furaha FM	Haki za ardhi, mabadiliko ya tabia nchi, na usalama wa chakula kwa wazalishaji wadogowadogo.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	22/07/2014

Furaha FM	Athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa mifugo na wafugaji	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	23/07/2014
Furaha FM	Athari za mabadiliko ya tabia nchi zinavyochochea wanavijiji kuhamia mijini.	Kimerekodiwa	Chiombola & Valentine	24/07/2014
Furaha FM	Utaratibu wa uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi nchini: Uzoefu kutoka wilaya ya Kilolo.	Kimerekodiwa	Chiombola	25/07/2014
Furaha FM	Kipindi cha Live Radio Furaha	Moja kwa moja	Tomitho & Nakamo	2/08/2014

Radio One	Nini Hatma ya Migogoro ya Ardhi nchini: Tathmini ya miaka 20 ya HAKIARDHI	Moja kwa moja	Joseph Chiombola	23/09/14
TBC TAIFA	Uwekezaji Mkubwa katika Ardhi na Mustakabali wa Wazalishaji wadogowadogo: Tathmini ya Miaka 20 ya HAKIARDHI	Moja kwa moja	Cathbert Tomitho & Subira Kibiga	24/09/14
WAPO FM	Uwekezaji katika ardhi za vijiji na haki za ardhi za wazalishaji wadogowadogo: Tathmini ya miaka 20 ya HAKIARDHI	Moja kwa moja	Chiombola & Marcelina Charles	24/09/14
WAPO FM	Masuala ya Muhimu yaliyoibuliwa na Kongamano la Kitaifa la Masuala ya Ardhi.	Moja kwa moja	Yefred Myenzi	30/09/14
Country FM	Athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye maisha ya wazalishaji wadogowadogo nchini	Moja kwa moja	Chiombola & Saad	11/12/14

Furaha FM	Umuhimu wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa Wazalishaji wadogowadogo.	Moja kwa moja	Chiombola & Valentin	11/12/14
Ebony FM	Umuhimu wa Majukumu ya Halmashauri ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji katika Usimamizi wa Ardhi ya Kijij	Moja kwa moja	Cathbert & Saad	12/12/14
Country FM	Haki za Ardhi kwa Wanawake kwenye Ardhi za Vijiji	Moja kwa moja	Valentin & Chiombola	12/12/14
Furaha FM	Kujibu Maswali ya Moja kwa Moja ya Wasikilizaji	Moja kwa moja	Cathbert Tomitho	13/12/14
Ebony FM	Kuzungumzia Mafanikio ya Programu ya Haki za Ardhi, Utawala na Mabadiliko ya Tabianchi	Moja kwa moja	Cathbert & Chiombola	15/12/14
Furaha FM	Taratibu za Uwekezaji katika Ardhi ya Vijiji	Moja kwa moja	Joseph Chiombola	16/12/14
Ebony FM	Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Nchini: Vyanzo, Mbinu na Taratibu za Utatuzi	Moja kwa moja	Yefred Myenzi	16/12/14
Furaha FM	Taratibu za Uwekezaji katika Ardhi za Vijiji kwa Mujibu wa Sheria za Ardhi.	Moja kwa moja	Joseph Chiombola	16/12/14

Vipindi vya televisheni vilivyo rushwa hewani vilikuwa;

Kituo TV	Mada	Aina kipindi	Washiriki	Tarehe
ITV	Mafanikio ya programu ya haki za ardhi, utawala bora na maliasili katika wilaya Kilolo na Mufindi.	Kimerekodiwa	Wanufaika wa programu wilaya za Kilolo na Mufindi.	14/07/2014
ITV	Taarifa ya mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi uliyowezeshwa na HAKIARDHI katika wilaya Kilolo na Mufindi.	Kimerekodiwa	Cathbert Tomitho	18/07/2014
ITV	Mafanikio ya programu ya haki za ardhi, utawala bora na maliasili katika wilaya Kilolo na Mufindi.	Kimerekodiwa	Wanakijiji kutoka wilaya Kilolo na Mufindi walionufaika moja kwa moja na kutoka na programu	14/07/2014
ITV	Taarifa ya mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi uliyowezeshwa na HAKIARDHI katika wilaya Kilolo na Mufindi	Kimerekodiwa	Joseph Chiombola	18/07/2014
ITV	Rasimu ya Katiba: Je imetoa ulinzi wa kutosha kwa Ardhi na Rasilimali za Taifa	Kipindi cha Live - Kipimajoto.	Yefred Myenzi-HAKIARDHI, Edward Porokwa-PINGOS, Pacience Mlowe-LHRC	18/07/2014
ITV	Rasimu ya Katiba: Je imetoa ulinzi wa kutosha kwa Ardhi na Rasilimali za Taifa	Kipindi cha moja kwa moja – Kipimajoto.	Yefred Myenzi-HAKIARDHI, Edward Porokwa-PINGOS, Pacience Mlowe-LHRC	18/07/2014

Channel Ten	Nini suluhisho la migogoro ya ardhi nchini?	Kipindi cha moja kwa moja – Baragumu.	Godfrey Massay & Valentine Ngorisa	23/07/2014
Channel Ten	Rasimu ya Katiba imezungumza nini kwenye masuala ya ardhi: Je inaweza kutatua migogoro ya ardhi nchini?	Kipindi cha kurekodiwa - Pambanua	Godfrey Massay na Valentine Ngorisa.	23/07/2014
Channel Ten	Nini suluhisho la migogoro ya ardhi nchini?	Kipindi cha moja kwa moja – Baragumu.	Godfrey Massay & Valentine Ngorisa	23/07/2014
Channel Ten	Rasimu ya Katiba imezungumza nini kwenye masuala ya ardhi: Je inaweza kutatua migogoro ya ardhi nchini?	Kipindi cha kurekodiwa-Pambanua	Godfrey Massay na Valentine Ngorisa.	23/07/2014
ITV	Awamu ya pili ya bunge la katiba izingatie mambo gani ili kupata katiba yenye tija kwa Taifa.	Kipindi cha moja kwa moja - Kipimajoto.	Joseph Chiombola-HAKIARDHI, Juvenile Rwegasira –WLAC, Buberwa Kaiza-FoDIA.	1/08/2014
ITV	Nini Kifanyike Kumaliza Migogoro ya Ardhi nchini Tanzania?	Kipindi cha moja kwa moja - Malumbano ya Hoja	Cathbert Tomitho kutoka HAKIARDHI alikuwa mmoja wa wageni walikwa.	14/08/2014
ITV	Awamu ya pili ya bunge la katiba izingatie mambo gani ili kupata katiba yenye tija kwa Taifa.	Kipindi cha moja kwa moja - Kipimajoto.	Joseph Chiombola-HAKIARDHI, Juvenile Rwegasira –WLAC, Buberwa Kaiza-FoDIA.	1/08/2014
ITV	Nini Kifanyike Kumaliza Migogoro ya Ardhi nchini Tanzania?	Kipindi cha moja kwa moja - Malumbano ya Hoja	Cathbert Tomitho – HAKIARDHI alikuwa mgeni mwalikwa.	14/08/2014

2.6.4 Usambazaji wa machapisho

HAKIARDHI inazalisha machapisho ya haki za ardhi kwa madhumuni ya kuongeza maarifa na uelewa juu ya masuala mbalimbali ya ardhi kwa jamii inayaofanya nayo kazi. Usambazaji wa machapisho hasa kufanywa kwa wazalishaji wadogo wadogo ambao ndio lengo kuu la programu za Taasisi katika kuwawezesha kuongeza sauti ya kilio cha pamoja kwa madai ya kushirikishwa katika vyombo vya maamuzi katika ngazi mbalimbali. Wanufaika wengine wa machapisho haya ni taasisi na mashirika mbalimbali yanayojihusisha na utetezi wa masuala ya ardhi nchini. Halikadhalika taasisi za serikali ni wanaufaika wakubwa wa machapisho haya ambayo huyatumia kwenye shughuli zao mbalimbali za uaandaaji wa sera pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Kwa mwaka 2014, machapisho iliyotolewa kwa umma ni kama ilivyoainishwa katika jedwali hapa chini;

SN	JINA LA CHAPISH0	IDADI
1.	Mwongozo wa Mafunzo	3,000
2.	Mwongozo wa Mafunzo (AAT)	900
3.	Mwongozo wa Mafunzo (Land Node)	15
4.	Ardhi iwe Nguzo katika Katiba	3,000
5.	Jarida la Kujielimisha (CARE)	4,000
6.	Jarida la Kujisomea (LIMAS)	55
7.	Maswali na Majibu Migogoro ya Ardhi	50
8.	Kilimo Kwanza	10
9.	Kamati ya Maamuzi- Poster	108
10.	Baraza la Kata –Poster	200
11	Baraza la Ardhi la Kijiji-Poster	150
12.	Mkutano Mkuu- Poster	300
13.	Mpango wa Matumizi- Poster	350
14.	Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro-Poster	100
15.	HAKIARDHI'S Brochures	200
16.	Citizens' Brief- (1-23) @900	20,700
17.	Policy Brief on Climate Change	150
18.	Fact Sheet on Climate Change	800
19.	Newsletter Volume 12.	1,500
20	Kalenda ya Mwaka 2015	2,000
	Jumla	**37,588**

SURA YA TATU

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KITENGO CHA UHUSISHWAJI JAMII

SURA YA TATU

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KITENGO CHA UHUSISHWAJI JAMII

3.1 UTANGULIZI

Kitengo cha Uhusishwaji Jamii kimeweza kutekeleza shughuli kwa mujibu wa mpango mkakati wa Taasisi wa 2012/2015 kama ifuatavyo;

3.2 PROGRAMU YA MAFUNZO YA HAKI ZA ARDHI NA UTAWALA VIJIJINI

Lengo Mkakati 1: Kukuza Uelewa wa Wanavijiji na Viongozi Kupitia Vyombo vya Utoaji wa Maamuzi katika Masuala ya Ardhi, Rasilimali, Mazingira na Mabadiliko ya Tabia nchi.
Katika kufikia lengo mkakati, utekelezaji wa mafunzo ya haki za ardhi na utawala vijijini umelenga kuwajengea uwezo wanavijiji na viongozi katika ngazi za serikali za mitaa kwa namna mbili. Kwanza, kuwaelimisha juu ya haki zao katika rasilimali ardhi katika wigo wa sera na sheria za ardhi nchini na pili, namna ambavyo wanaweza kuwajibika katika usimamizi bora wa ardhi na rasilimali kupitia vyombo vya utoaji maamuzi kutokana na elimu waliyoipata ili kuhakikisha haki zao katika ardhi zinalindwa na wanaitumia kwa maslahi yao kijamii na kukuza uchumi wao. Katika Kipindi hiki mafunzo yamefanyika katika wilaya za Mkuranga, Morogoro vijijini, Ulanga, Kilolo, Mufindi, Mkinga na Kilindi kama kiambatanisho A cha ripoti hii kinavofafanua.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA MAFUNZO YA HAKI ZA ARDHI KWA VIONGOZI NA WANANCHI

TAREHE	WILAYA NA NGAZI YA MAFUNZO	USHIRIKI	MASUALA YALIYOJITOKEZA
1 7 - 19/3/2014	Viongozi wa kijiji cha Vihengele (Morogoro)	-**45** (**15** Ke) kati ya washiriki **50** waliokusudiwa. -Wafadhili kutoka Austria ambao ni (Horizon 3000 na Welthaus).	-Uelewa mdogo wa majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji na Halmashauri ya Kijiji. -Migogoro ya ardhi iliyo na mizizi ya operesheni vijiji na gharama kubwa zinazotozwa katika uendeshaji migogoro ya ardhi katika baraza la Kata. -Usimamizi wa ardhi katika wilaya ni hafifu na unaitaji watendaji na bajeti kuwawezesha katika usimamizi wa ardhi hususani matumizi ya ardhi ambayo kwa vijiji vingi vya Morogoro umefanywa na wafadhili. -Wafadhili walifurahishwa na mafunzo na vitini vilivyotolewa ambavyo walishauri kualika vijiji jirani pia nje ya mradi wakati wa mafunzo mengine kwa vijiji 14 vilivyobakia.
6-7/5/2014	Watendaji wa wilaya ya Mkuranga: Idara ya ardhi, maliasili, maendeleo, wenyeviti na watendaji wa vijiji na wenyeviti wa mabaraza ya ardhi ya vijiji 15.	-**49** (**5** Ke) kati ya washiriki **50** waliokusudiwa.	-Wanavijiji na viongozi kuuza maeneo kwa wawekezaji na kwa wageni hususan kutoka Dar ambao hawaendelezi ardhi inavyopaswa. -Mabaraza ya utatuzi wa migogoro ya ardhi hutoza gharama kubwa kwa wananchi ambapo mwanasheria wa wilaya na mwakilishi wa baraza la ardhi la wilaya hii waliomba ushirikiano kutoka kwa Taasisi kutatua changamoto hii wakati wa Mafunzo.

1 5 - 16/5/2014	Watendaji wa wilaya ya Ulanga: Idara ya ardhi, maliasili, maendeleo, wenyeviti na watendaji wa vijiji na wenyeviti wa mabaraza ya ardhi ya vijiji 15	**54** (**9** Ke) kati ya washiriki **50** waliokusudiwa.	-Maafisa ardhi walilalamikia bajeti ndogo katika idara ya ardhi ambayo imechangia kutopanga matumizi kwa vijiji, kutoa mafunzo kwa vyombo mbalimbali katika vijiji ikiwemo halmashauri na mabaraza ya ardhi ya vijiji. Matokeo yake yamesababisha matatizo mengi ya ardhi yanayoletwa na wananchi katika wilaya kuchukua muda mrefu kutatuliwa au kutotatuliwa kama wananchi wanavotarajia. -Baadhi ya washirki waliwalalamikia wananchi wanaoharibu alama za mipaka katika baadhi ya vijiji kama vile Kilosa Mpepo, Malinyi na Ihowanza mjadala ambao waliazimia viongozi wa vijiji hivo wajitahidi kusuluhisha migogoro ya mipaka. -Mafunzo kwa washiriki hawa yaliweza kusaidia kutofautisha majukumu ya kamati ya uamuzi ya Kijiji na kamati zingine vijijini jambo ambalo washiriki walikua wakichanganya majukumu baina ya vyombo hivi.
27 Mei – 4 Jun 2014	Viongozi wa vijiji kutoka vijiji 14 vya wilaya ya Morogoro vijijini.	**616** (**217** ke) kati ya **700** waliokusudiwa kupata mafunzo	-Kijiji cha Dete na Kisanga Standi kiliagiza wilaya kuwaambia RUDABA kuwa hawajawapatia maeneo na hivo utaratibu wa kufika Kijijini na kutenga maeneo ya uwekezaji ni kinyume na utaratibu. -Ongezeko la migogoro ya wakulima na wafugaji katika vijiji vya Mkuyuni, Kungwe na Kifindike. -Vijiji vyote vina migorgoro ya mipaka baina yao na vijiji vinavyo pakana nje na vilivyopatiwa Mafunzo. -Vijiji vya Tandai na Kitungwa havina mabaraza ya Kata na vilivyo na chombo hiki ni mara yao ya kwanza kupatiwa mafunzo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. -Washiriki hawafahamu chombo kitwacho kamati ya uamuzi ya kijiji katika masuala ya ardhi hivyo masuala ya ardhi yahusuyo uamuzi wa kiutawala katika halmashauri zao hufanywa na kamati ya maendeleo ya jamii.

9 – 18 Jun 2014	Viongozi wa vijiji wilaya ya Mkinga na Kilindi	**736** (**269** ke) kati ya **750** waliokusidiwa kupata mafunzo Kilindi na Mkinga ni **685** (**266** ke) kati ya **750** walipatiwa mafunzo	-Vijiji vingi vilikuwa na migogoro ya mipaka na chanzo kikubwa kilichobainishwa ni uundwaji wa vijiji vipya ambayo mchakato wake haukueleweka vema kwa wananchi na pia ukosefu wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji ambapo hali hii hufanya mipaka ya vijiji kuwa ngumu kuibaini. -Migongano ya matumizi ya ardhi baina na watumiaji kutokana na mifumo ya uzalishaji na upatikanaji wa ardhi. Kuna baadi ya vijiji vina wakulima na wafugaji na vina migororo kutokana na ukosefu wa ardhi kukidhi mfumo wa kifugaji wa wafugaji hivyo kuingilia maeneo ya kilimo na mengineyo ambayo sio yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji -Kilindi imejaliwa madini ya rubi na dhahabu hususani katika vijiji vya Kigunga, Masagalu, Muheza na Mtolo. Wakufunzi walipata malalamiko kutoka kwa washiriki kuhusiana na kutonufaika na uwekezaji wa madini lakini pia ardhi yao kuchukuliwa pasipo ushirikishwaji wao na kuathiri ulipwaji wa fidia pia -Wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya vijiji na ya Kata hayana uelewa wa utekelezaji wa majukumu yao na maadili wakati wa utatuzi wa migogoro ya Ardhi. -Ushiriki hafifu wa wanawake katika vyombo vya utoaji maamuzi ila pia wakati wa mafunzo ushiriki wao katika mijadala ulikuwa wa chini sana na wakufunzi waliweza kusisitiza nafasi ya wanawake katika kumiliki ardhi na rasilimali.

12– 22 Aug 2014	Wanavijiji wa kawaida wilaya ya Morogoro	**750** (**375** ke) ushiriki uliokusudiwa ulifikiwa	-Ardhi ya vijiji vya Kifundike, Kiswila na Kitungwa inamilikiwa na kanisa Katoliki hivyo kuwafanya wanavijiji kutopata fursa ya kumiliki ardhi na kuathiri mifumo ya uzalishaji kwani kanisa limewapa asharti ya kutolima mazao ya kudumu na kutokuuza ardhi. Wananchi waliomba mwakilishi wa wilaya kwa kushirikiana na wilaya kumwandikia kamishna wa ardhi ombi la kutengua hati hiyo mana ni ya muda mrefu sana ili waweze kumiliki maeneo hayo. -Migogoro ya ardhi baina ya wamiliki wa zamani na waliopo inayochangiwa na matukio ya hamisha hamisha wakati wa operesheni vijiji. Hii imeelezewa na vijiji vya Tandai, Kibwaya na Kungwe ambapo kuna migongano katika matumizi ya ardhi baina ya wamiliki wa liopo na wale wa kabla ya operesheni vijiji. Suala hili lilibainishwa na wakufunzi na washiriki kupatiwa ushauri. -Wanavijiji hawafahamu majukumu ya mkutano mkuu wa kijiji na hadhi ya maamuzi wanayoyafanya kupikia mikutano hiyo bali wanakitazama kama chombo kinachotakiwa kutoa maamuzi ya kukubaliana na kile ambacho wanaambiwa kutoka ngazi za juu. Ushiriki pia umekuwa ukisuasua katika mikutano mathalani idadi ndogo ya ushiriki ilionekana katika kijiji cha kitungwa ambapo wananchi 52 tu walihuduria mkutano wa kijiji mwezi Juni 2014 -Mgogoro baina ya wanavijiji na serikali yao ya kijiji kuhusu maeneo waliopatiwa na serikali kipindi cha nyuma miaka ya 1999. Serikali imekuwa ikiwataka werejeshe maeneo hayo ambayo walipewa kwa muda wanavijiji wanadai walipwe fidia. Mgogoro huu upo mahakamani.

8 – 1 8 / 1 0 / 2014	viongozi wa vijiji kutoka wilaya ya Ulanga na Mkuranga	**703** (**255** ke) kati ya **750** waliokusidiwa kupata mafunzo Mkuranga na Ulanga ni **750** (**269** ke) kati ya **750** walipatiwa mafunzo	-Mafunzo ya sheria za ardhi, usimamizi rasilimali na utawala pamoja na utatui wa migogoro ya ardhi yalitolewa. -Katika baadhi ya vijiji kwa wilaya zote 2 vimeunda mabaraza ya ardhi ya vijiji toka kushauriwa wakati wa utekelezaji wa utafiti wa awali (*baseline study).* -Wilaya ya Mkuranga imesitisha zoezi la mpango wa matumizi ya ardhi vijijii uliokuwa ufanywe na RUBADA kutokana na uhalisia kwamba unafanyika kwa maslahi yao wenyewe na wawekezaji wa nje. -Wanavijiji wamekiri kwamba mafunzo yaliyofanyika awali kwa viongozi yameboresha utendaji wa vyombo mbalimbali vya utawala vijijini.
2 3 / 1 0 - 2 /11/2014	Ngazi ya wanavijiji wa kawaida kutoka wilaya ya Kilindi na Mkinga	Kilindi **750** (**350** ke), Mkinga **750** (**356** ke) Idadi kusudiwa ilifikiwa ya 750 kila wilaya, vijiji 15 kwa uwiano wa washiriki 50 kwa kijiji	-Washiriki walifundishwa mfumo wa milki ya ardhi na umuhimu wa vyombo vya usimamizi rasilimali vijijini na utatuzi wa migogoro ya ardhi -Washiriki walikiri mabadiliko ya mfumo wa utawala vijijini uliofanywa na viongozi wao waliokwisha pata mafunzo kabla yao -Baadhi ya washiriki walijitolea kutoa elimu kwa wenzao baada ya mafunzo -Ushiriki wa wanawake katika maamuzi umeimarika. -Uitishwaji wa mikutano ya vijiji katika vijiji vya Mapatano, Machimboni na Perani kutoka wilaya ya Mkinga vimeitishwa ukilinganisha na kipindi cha nyuma ambapo ilikua haifanyiki -Kwa ujumla katika ngazi hii ya mafunzo masuala ya mabadiliko ya utendaji wa usimamizi rasilimali na utawala yamepiga hatua

1 4 - 18/12/2014	Waangalizi wa masuala ya ardhi kutoka wilya ya Kilolo na Mufindi	**40** (**20** Ke) kati ya **40** waliokusidiwa	-Mafunzo yaliweza kuwapatia waangalizi uelewa wa mfumo wa umilikaji ardhi nchini, mamlaka za utawala katika usimamizi wa ardhi, namna ya kutoa elimu ya masuala ya ardhi pamoja na harakati za kusaidia jamii katika masuala ya ardhi -Masuala yaliyojitokeza na kujadiliwa ni pamoja na matatizo ya mirathi inayohusisha ardhi, malalamiko kuhusu uitishwaji wa mikutano kutofanyika ipasavyo, na mamuzi ya wanavijiji kuhusu ardhi na rasilimali za vijiji kuingiliwa na viongozi na wanasiasa. -Maazimio yaaliyofikiwa ni pamoja na waangalizi kushughulikia masuala ya ardhi vijijijni na kuendeleza elimu waliyoipata. -Waliweza kuomba mafunzo ya pamoja na waangalizi 60 wa vijiji vingine kwa lengo la kutambuana na kupeanan uzoefu wa harakati za masuala ya ardhi vijijini mwao.
13 -18/11/ 2014	Mrejesho wa utekelezaji wa program Wilaya ya Kilolo na Mufindi	Washiriki 30 kwa kila wilaya (DED, wenyeviti wa halmshauri, madiwani, maafisa ardhi, mipango, uthamini, maliasili, upimaji, mazingira, maendeleo, kilimo, mwanasheria, na waangalizi wa masuala ya ardhi)	-Warsha hizi zilifanyika katika kumbi za wilaya husika. -Lengo ni kutoa mrejesho wa utekelezaji wa program nzima ikiwa ni pamoja na kuazimia kwa pamoja namna ya kutatua changamoto za masuala ya ardhi yaliyojitokeza katika kipindi cha programu. -Washiriki walishukuru Taasisi kwa kazi waliyoifanya ya mafunzo, tafiti, vipindi vya redio/runinga, mijadala ya wazi, ushauri wa kisheria na mpango wa matumizi ya ardhi hadi kufikia kutoa hatimiliki kwa baadhi ya vijiji. -Kwa wilaya ya Mufindi DED aliomba radhi kwa usumbufu taasisi iliopata wakati wa utekelezaji wa program na kuaidi kutoa ushirikiano pale taasisi itakapo kuwa inatekeleza programu nyingine.

3.3 UCHAMBUZI WA SHERIA ZA ARDHI NA MIJADALA NA WADAU KATIKA MASUALA YA ARDHI NA RASILIMALI

Lengo Mkakati 2: Uboreshaji wa mfumo wa sheria za ardhi kulinda milki za wazalishaji wadogo

3.3.1 Uchambuzi wa rasimu ya Katiba na Baraza la Katiba la Taasisi

Tarehe 5-9 Mei, 2014 Mkurugenzi pamoja na afisa programu kutoka Kitengo cha Uhusishwaji jamii walifanya kikao mjini Dodoma na baadhi ya wabunge kutoka kundi la 201 kwa lengo la kuwashirikisha masuala muhimu ya ardhi kuingizwa katika katiba. Masuala hayo ambayo ni nyaraka ambayo Taasisi ilikua imeandaa, ilipokelewa vizuri na wabunge hao ambao waliaidi kuitumia katika majadiliano katika kamati na pia katika mijadala ya Katiba Bungeni.

Kwa kuwa Bunge la Katiba limesitishwa kupisha Bunge la Bajeti mpaka mwezi Agosti, taasisi imepanga kufanya uchambuzi wa taarifa za kamati na mijadala ya Bunge kuweza kubaini na kuainisha namna ambavyo masuala ya ardhi yalijitokeza au kutetewa na wabunge. Uchambuzi huu utasaidia taasisi kuweza kuendeleza ushawishi katika Bunge la Katiba

3.3.2 Uchambuzi wa Katiba pendekezwa

Tarehe 27- 28/11/2014 Taasisi ilifanya uchambuzi wa Katiba pendekezwa katika ukumbi wa Kibaha ambapo wafanyakazi walishiriki. Lengo la uchambuzi huo ilikua ni kuanisha

maeneo ya utetezi katika masuala ya ardhi na rasilimali ambayo yatatumika katika kusaidia jamii kuelewa rasilimali ardhi kabla ya kura ya maoni.

Uchambuzi huu uliweza kuanisha namna ambavyo uhakika wa ardhi, ukomo wa umiliki, kiwango cha umiliki mtu anaweza kumiliki unapaswa ujitokeze katika Katiba. Pia kundi la waokota matunda ambalo halikuwepo liliongezwa pamoja na masuala ya kuhodhi ardhi yalibainishwa. Uchambuzi huu utakamilika baada ya azimio la idara ya utawala na programu kuitisha kikao baina ya wafanyakazi na wanachama wa taasisi ili kuikamilisha kabla haijasambazwa kwa wadau wengine wenye mrengo wa Taasisi.

3.3.3 Msaada wa kisheria katika masuala ya ardhi

Taasisi imeweza kutoa msaada wa kisheria katika masuala ya ardhi kwa wananchi wenye uhitaji huo kama ifuatavyo

3.3.3.1 Wananchi waliopata usaidizi wa kisheria ofisini

Mwaka huu jumla ya wananchi Taasisi imepokea jumla ya wananchi wapatao 73 (26 Ke) waliohitaji msaada wa kisheria katika nyanja mbalimbali kama vile masuala ya fidia, mirathi, umiliki, taratibu za kufungua madai, namna ya kujitetea mbele ya vyombo vya sheria, mipaka, migogoro ya ardhi baina ya ndugu, ipo ya wananchi na taasisi za dini, migogoro ya umiliki na uvamizi wa maeneo ambayo yote kwa ujumla walisaidiwa. Idadi tajwa hapo juu ni wananchi 48 (13 Ke) ndio waliofika ofisini moja kwa moja na wengine ni kwa njia ya simu msaada wa kisheria ulitolewa kwao.

Maeneo walipotokea wananchi hawa ni pamoja na Sinza, Mara, Bagamoyo, Kinondoni, Kigamboni, Dodoma, Kilolo, Turiani, Mulbadaw na Tandika. Vilevile katika usaidizi huu wa kisheria kulikuwa na uwakilishi wa mahakamani kwa kesi ambazo taasisi iliona zina umuhimu wa kufaya hivyo na wakili Shilinde Ngalula kutoka Kituo cha Haki za Binandamu -Arusha alipewa jukumu hili katika kesi ya Zacharia Joseph, Joel Shauri, Petro Tarimo, Paul Fiay na wengine 147 dhidi ya Christina Mndeme na wengine 8 (Kesi No.44/2014) ambapo wakili aliweza kuibua hoja ya mapungufu ya kisheria katika kesi hiyo na kupelekea mahakama kufuta kesi

3.3.3.2 Msaada wa kisheria katika wilaya za programu

- Katika nyakati tofauti ushauri wa Kisheria katika wilaya za Programu ulitekelezwa katika Kipindi hiki. Wilaya hizo ni Kilolo na Mufindi ambapo kwa wilaya ya Kilolo wananchi wapatao 40 (16 ke) Kutoka vijiji vya Kitalamwa, Kimala, Kisima, Ndengisivile na Mwatasi walisaidiwa kisheria katika masuala yao ya ardhi kuanzia tarehe 10-14 Februari, 2014. Kwa upande wa wilaya ya Mufindi kuanzia tarehe 4-8 Februari, 2014 jumla ya wananchi 40 (9 ke) kutoka vijiji vya Kisasa, Iramba, Mangunguli, Wambimbalwe na Mbalamaziwa walisaidiwa kisheria katika masuala ya ardhi. Masuala yaliyotolewa ushauri kwa wilaya zote mbili yalihusu masuala ya mirathi ya ardhi kwa wanawake pale wanapoachwa, migogoro ya mipaka baina ya wananavijiji na migogoro ya mali katika familia na migongano ya mauziano ya mashamba baina ya wananchi.

- Pia kati ya tarehe 22- 30 Juni, 2014 na 9-18 Disemba, 2014 vijiji vya Kising'a, Makungu, Mkaranga, Kitumbuka, Lugalo, Ikuka na Uhambingeto wilaya ya Kilolo vilipata fursa zaidi ya utolewaji wa msaada wa kisheria kutokana na maombi ya wananchi kwa vijiji mbalimbali kuomba usaidizi huo. Vijiji hivyo vilikuwa ni; Ilutila, Madege, Mhanga, Lugalo, Uhambingeto, Mazombe, Mlafu, Kising'a, Makungu, Mkaranga, Kitumbuka, Lugalo, Ikuka na Uhambingeto. Jumla ya wananchi 141 (42 ke) walisaidiwa katika masuala ya fidia na taratibu zake, migogoro ya mipaka na mashamba baina ya wanavijiji na vijiji. Migogoro ya aina hii afisa ardhi alisaidiana na wanasheria wa taasisi kutoa mwongozo. Masuala mengine waliosaidiwa wananchi ni pamoja na taratibu za umiliki na upatikanaji wa ardhi kwa wanawake.

Katika shughuli zote hizi, wanasheria wa taasisi sio tu waliwapatia ushauri wa kisheria ila waliweza kuwaelimisha pia juu ya masuala waliyoyawasilishwa kwa uelewa zaidi ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji maagizo wanayopatiwa.

3.4 USHIRIKI WA TAASISI NA JAMII JUU YA MASUALA YA ARDHI

Lengo Mkakati 3: Kuelimisha jamii kutambua haki zao katika ardhi na umuhimu wa kushiriki na kujadili masuala ya ardhi kupitia vyombo vya utoaji wa maamuzi

3.4.1 Mijadala ya wazi katika wilaya za programu kuhusiana na haki za ardhi, utawala vijijini na mabadiliko ya tabianchi

3.4.1.1 Mijadala ya wazi katika wilaya za Kilolo na Mufindi

Mijadala ya wazi katika wilaya zote mbili ilifanyika katika wilaya ya Kilolo na Mufindi na ilihusu mifumo ya umilikaji ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na mazingira kuanzia tarehe 3-15 Februari, 2014 katika vijiji vitano kwa kila wilaya. Vijiji hivyo ni pamoja na Magunguli, Wamimbalwe, Kisasa, Iramba na Mbalamaziwa kwa wilaya ya Mufindi na Kitalamwa, Kimala, Kisima, Ndengisivile na Mwatasi kutoka wilaya ya Kilolo. Jumla ya washiriki 921 (364 ke) kutoka vijiji vya wilaya ya Kilolo walihudhuria na kwa wilaya ya Mufindi jumla ya washiriki 570 (237 ke) walihudhuria mijadala ya wazi.

Masuala muhimu yaliyoibuka katika wilaya zote ni pamoja na malalamiko ya wanawake kuhusiana na mgawanyo wa mali za mirathi ambapo mila za wahehe zimekuwa zikiwakandamiza. Pia masuala ya rushwa katika ardhi yalitajwa na viongozi wa vijiji kuonekana vinara katika jambo hili pamoja na matumizi mabaya ya madaraka ya uongozi ambapo ardhi nyingi zimeuzwa kinyume na utaratibu uliowasilishwa na wakufunzi wa taasisi wakati wa mijadala.

Washiriki waliomba taasisi iendelee na mijadala hii kwa wilaya nzima lakini pia kuongeza idadi ya vitini ili wananchi wengi wapate. Ukilinganisha na mijadala iliyopita katika wilaya hizi idadi imekua ikiongezeka katika vijiji wanaposikia taasisi inatarajia kufanya mijadala ya wazi juu ya masuala ya ardhi na mazingira.

Picha 5: Wananchi wakishiriki kwenye mjadala wa wazi wilayani Kilolo na Mufindi

Vilevile tarehe 22 - 30 Juni 2014 wilaya Kilolo ilifanyika mijadala ya wazi juu ya Masuala ya Ardhi na Mabadiliko ya tabia nchi katika vijiji 7 ambavyo ni; Ilutila, Madege, Mhanga, Lugalo, Uhambingeto, Mazombe na Mlafu. Jumla ya wananchi wapatao 689(320 ke) walihudhuria. Wakati wa mijadala wanavijiji wawili wa kijiji cha Lugalo; Melina Mnyagala na Alubertha Mnyagala walikiri kusikiliza vipindi vya redio ambapo walipata elimu juu ya masuala ya mirathi na

waliweza kusaidia kutoa ufafauni kwa wanakijiji wakati wa mjadala.

Kijiji cha Uhambingeto kilikiri kuwa walihamasishwa na uelewa wa masuala ya ardhi kwa wananchi wa kijiji cha kipaduka ambapo wameweza kufikia hatua ya kufanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi hivyo mjadala katika kijiji hiki wanavijiji na viongozi walidhamiria kuzingatia na kuitumia elimu waliyopata kwa ajili ya matumizi endelevu ya ardhi yao.

Pia katika vijiji vya Uhambingeto, Mlafu, Ilutila na Madege iligundulika kuwa watendaji ngazi ya kitongoji walihusika katika kugawia wananchi maeneo pamoja na kutatua migororo ya ardhi kinyume na utaratibu hivyo wananchi na viongozi waliofika katika mijadala hiyo waliweza kupatiwa elimu ya vyombo vinavyohusika katika ugawaji wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Suala la uwekezaji lilijitokeza katika kijiji cha Mdege ambapo kulifanyika mradi wa kupitisha umeme na toka 1993 kuna wananchi wapatao 25 hawajapatiwa fidia zao. Afisa ardhi wa wilaya alisaidia kutoa mrejesho kwamba vikao vilivyokuwa vinafanyika viliamuru fidia hiyo ilipwe. Ilibainika vijiji karibu vyote havina kamati ya maanuzi ya kijiji inayoshughulikia masuala ya ardhi na kiutawala kupitia halmashauri za vijiji. Vijiji vya Mlafu na Lugalo vina migogoro ya mipaka japo wilaya ilishafanya mpango wa matumizi ya ardhi.

Awamu nyingine ilihusisha vijiji vitano kila wilaya na mijadala ilifanyika tarehe 2-7 Septemba 2014 Kilolo na tarehe 9 - 13 Septemba 2014 kwa wilaya ya Mufindi. Wilaya ya Kilolo vijiji vilikuwa ni Ilutila, Madege, Idasi, Masisiwe na Nyawegete na wanavijiji wapatao 1180(431 ke) walihudhuria. Wilaya ya Mufindi ni vijiji vya Kibada, Kipanga, Ilogombe,

Nyakipambo na Ipilimo ambapo jumla ya wanavijiji wapatao 1119(480 ke) walihudhuria.

Masuala yaliyoibuka ni pamoja na migogoro ya mipaka, migongano ya ugawaji mali inayohusisha ardhi katika suala la mirathi ambapo mila imekuwa ikizingatiwa zaidi, ilibainika uuzaji wa ardhi upo katika vijiji vyote. Pia vyombo vya usimamizi wa ardhi katika vijiji hivi vinaitaji mafunzo zaidi maana majukumu mengi kwa mujibu wa sheria yalionekana kutofahamika au kueleweka hususani katika utekelezaji wake.

Picha 6: Wananchi wa kijiji cha Ipilimo, Mufindi wakishiriki katika mjadala wa wazi

3.5 USHIRIKIANO NA TAASISI KITAIFA

Lengo Mkakati 5: Kukuza uelewa na mashirika mengine ngazi ya kitaifa na kimataifa juu ya masuala ya ardhi na rasilimali.

TAREHE	ENEO	MADA	WASHIRIKI	MASUALA YALIYOIBUKA
16 -18 /4/2014	Morogoro MVIWATA	Siku ya kuenzi wakulima duniani	Saad Ayoub na Frank Madenge - mwangalizi Mgugwe, Kilombero	- Wakulima walitoa madai mbalimbali kwa serikali na wadau wengine hususani asasi za kiraia. Baadhi ya madai hayo ni kupimwa kwa maeneo ya kilimo Ili kupunguza migongano ya kimatumizi na wafugaji, serikali kurejesha ardhi zilizotelekezwa na wawekezaji au kuchukuliwa kinyume na sheria kwa wananchi ili zitumike kwa ajili ya kilimo na pia serikali iwawezeshe fursa za masoko, mitaji, pembejeo na miundombinu itakayaoboresha kilimo na maisha yao kwa ujumla.
23/4/2014	Dar es salaam -LHRC	Uzinduzi wa ripoti ya Haki za Binadamu 2013	Nakamo Tenende	- Ripoti imebainisha ongezeko la ukiukwaji wa haki za binadamu ukilinganisha na miaka iliyopita. Pia ripoti iliweza kubaini hotuba za viongozi ambazo pia zilichochea ukiukwaji wa haki za binadamu. Mfano wa hotuba hizo ni pamoja na ya Waziri Mkuu iliyochangia ukiukwaji wa haki za binadamu katika *Operesheni Kimbunga na Operesheni Tokomeza Ujangili* nchini.
28/4/2014	Dar es Salaam	Miaka 20 ya LEAT	Nakamo Tenende	-Taasisi pamoja na asasi zingine zilizofanya kazi na LEAT ziliweza kusikia mafanikio ya LEAT toka ianzishwe katika masuala ya mazingira pamoja na changamoto walizokumbana nazo kama vile ukosefu wa rasilimali watu na fedha katika shughuli zao za ushawishi na utetezi pamoja na ushirikiano mdogo kutoka kwa serikali kwa baadhi ya shughuli walizofanya.

5/8/2014	Dar es Salaam	Mkutano wa ulioandaliwa na bodi ya usajili na mipango miji kuhusu kasi ya ukuaji wa miji holela na nini kifanyike	Joseph Chiombola	-Mkutano huu uliudhuriwa na wadau wa wizara ya ardhi, kilimo, wafugaji, wananchi, idara za ardhi za wilaya, manispaa na asasi za kiraia. -Changamoto kubwa iliyobainishwa pamoja na uwepo wa sheria za mipango miji ni ongezeko la watu mijini wakati kasi ya urasimishaji na mipango ya ardhi mijini ikilegalega. -Washiriki waliweza kukubaliana kuwepo kwa mfumo mpya wa makazi utakaosaidia changamoto hiyo. -Pia kutatua suala la usimamizi wa ardhi mijini ambapo kumekuwa na mkanganyiko wa mamlaka baina ya viongozi wa mipango miji na viongozi wa mitaa. -Kuna migogoro ya ardhi mingi katika maeneo yaliyopimwa, ama wakati wa upimaji na pia maeneo yasiyopimwa -Kuna haja ya kuipa sekta ya upimaji kipaumbele ilibainishwa ikiwa ni pamoja na wananchi kupatiwa elimu ya usimamizi wa ardhi kufuatilia maeneo yao ili kila maendelezo yanayofanywa yaweze kuendana na ramani ya eneo husika ikiwa ni pamoja na kushirikiana na sekta zingine. -Pia wizara ya ardhi ishirikiane na wadau wengine kufanya tafiti na uchambuzi wa sheria zilizopo kuhusu mipango miji ili kuziboresha zaidi.
13-14/8/2014	Dodoma	Semina kuhusu maudhui ya Rasimu ya kwanza ya Katiba	Joseph Chiombola	-Semina iliweza kutoa elimu juu ya mchakato wa katiba na rasimu iliyotoka kwa washiriki ambao wengi walikuwa ni asasi za kiraia. -Semina hii iliazimia washiriki wakatoe elimu juu ya rasimu hiyo kwa wananchi pamoja na kufanya mijadala mbalimbali ya kuichambua ili maslai ya wanyonge yakabainishwe.

25-26 /9/ 2014	Dar es Salaam	Kongamano la Kitaifa juu ya masuala ya ardhi (NALAF)		-Kongamano la kitaifa ililihusu masuala ya ardhi ambapo watu wa aina mbalimbali walishiriki. Jumla ya washiriki **130** (**70** ke) waliudhuria kutoka Dar, mikoani na nje ya nchi kama: KLA-Kenya, ULA-Uganda na AIAS-Zimbabwe. -Lilikuwa mahususi kwa ajili ya kujadili dhima isemayo ***"mabadiliko katika mfumo wa milki ya ardhi na hatma ya wazalishaji wadogo Tanzania: tathmini ya miaka 20 ya harakati"*.** Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na maeneo ya ardhi za vijiji na wanavijiji kuporwa na wawekezaji. -Utungaji na uwepo wa sera na sheria za ardhi pamoja na marekebisho yake yasiyomnufaisha mzalishaji mdogo. -Vilevile kongamano hili liliweza kutoa visa mkasa ambavyo viliweza kuonesha umuhimu wa ardhi kama rasilimali ya msingi sana kwa mzalishaji mdogo. Uzoefu wa harakati kutoka nje ya nchi nao ulibainisha masuala ya ardhi yanayofanana na Tanzania kama vile migogoro ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji, baina ya wananchi, ukosefu wa sera ya makazi mbadala, makazi duni, mabadiliko ya tabia nchi, ukosefu wa elimu na taarifa za ardhi katika jamii ikiwemo serikali. -Maazimio yaliyofikiwa ni pamoja kuanzisha mfuko wa ardhi, kuendelea kufanya tafiti na uchapishaji wa taarifa mbalimbali za ardhi na kuzisambaza, kuendelea kujenga nguvu ya pamoja na wadau wenye mlengo unaofanana na taasisi pamoja na kuendeleza vipindi vya radio na televisheni. -Kongamano hili liliweza kurushwa hewani katika kipindi chote na vyombo vya habari kama vile TBC1, ITV, Channel Ten, Star TV, Radio One, TBC Taifa na WAPO Radio.

19-23/1/2015	Zimbabwe	Summer school	Gloria Jimwaga & Joseph Chiombola	-Mkutano ulihusu uwasilishaji wa mada mbali mbali zinazohusiana na sera za kilimo, hali ya wakulima na changamoto wanazopitia kutokana na mifumo ya siasa uchumi. -Washiriki wapatao 50 kutoka nchi mbalimbali kama vile Tanzania, Zimbabwe, Zambia, Angola, Kenya, Ghana, Senegali, Mali, Afrika Kusini, Botswana, Japani, Marekani, Brazil na India waliudhuria. -Maazimio yaliyofikiwa ni pamoja na kuendeleza ushawishi na utetezi wa maslahi ya wakulima hasa waishio vijijini ili kutatua changamoto zao. -Umuhimu wa kufanya rasilimali ardhi kuwa agenda kuu katika mijadala mbalimbali ili kuzuia uporaji wa ardhi ambao umekuwa tishio hasa kwa wakulima wadogo wenye kipato kisichotosheleza. -Katika msimu mwingine 2016 washiriki waliombwa na waratibu wakusanye fedha ili kuongeza ushiriki zaidi wa watu lakini pia kufanya tafiti mbalimbali kuhusu wakulima na siasa za uchumi za nchi zao.

3.5 KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA MTANDAO WA MASUALA YA ARDHI TANZANIA (TALA)

Lengo Mkakati 6: Kutandaa na kuboresha ushirikiano na asasi za kiraia kupitia Mtandao wa Mashirika yanayojishugulisha na masuala ya ardhi nchini (TALA)

3.5.1 Mijadala ya wabunge

Taasisi imeendelea kutoa ushauri wa kisheria na kifedha kwa kamati ya wananchi ya Kigamboni kupitia TALA. Mpaka sasa Kamati imeweza kutambuliwa na watekelezaji wa mradi huo pamoja na viongozi mbalimbali. Pia madai yao yameweza kusikika kwa wadau hao na wananchi kwa ujumla kupitia vyombo vya habari. Tarehe 21-31/5/2014 baadhi ya wajumbe wa Kamati hii waliwezeshwa kwenda Dodoma kwa lengo la kukutana na wabunge wa Dar es salaam, wabunge wenye maeneo Kigamboni na wabunge wanaounda Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira ili kuendeleza mijadala ya madai yao kwa niaba ya wananchi. Madai hayo ni pamoja na mradi kusitishwa kwa kuwa wananchi hawajashirikishwa ipasavyo na pia kuwepo na uwazi katika utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na suala la elimu na mchakato wa mradi kwa ujumla ufanyike kwa wananchi watakaoathirika. Dai lingine ni pamoja na wananchi kutotolewa katika maeneo yao.

3.6 UTEKELEZWAJI WA MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI VIJIJINI

Lengo kuu la utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi vijijini ni pamoja na kukabilinana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo wanavijiji wengi wamekuwa hawatumii maeneo yao na kubadilisha mifumo ya uzalishaji hivyo mpango utasaidia kuilinda pamoja na namna ya kufanya kilimo katika maeneo yao kukabiliana na mabadiliko hayo. Pia maeneo yenye migogoro ya ardhi na uporaji wa ardhi au uwekezaji mkubwa mpango wa matumizi ya ardhi unasaidia kuhakikisha ardhi za wanyonge haziporwi au kurubuniwa.

3.6.1 Uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kijiji cha Magunguli na Wamimbalwe wilaya ya Mufindi

Uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji hivi ulifanyika kwa pamoja kuanzia tarehe 19 Mei - 30 Juni 2014 ambapo Saad Ayoub alishiriki kwa niaba ya Taasisi kwa kushirikiana na kamati ya matumizi ya ardhi ya wilaya na vijiji husika. Masuala yaliyobainishwa wakati wa utekelezaji wa matumzi ya ardhi kwa vijiji hivi ni pamoja na uwepo wa migogoro ya mipaka ambayo iliweza kutatuliwa vema, uharibifu wa mazingira kama vile uchomaji misitu na kuharibu vyanzo vya maji na njia. Vijiji vyote walipewa elimu na kanuni ziliwekwa na wananchi wa vijiji husika ili kulinda mazingira. Pia kulionekana kuna uuzaji mkubwa wa maeneo na bei ya soko lake kupanda mara kwa mara hivyo mpango wa matumizi ya Ardhi uliyofanywa umesaidia kudhibiti hali hii ambayo baadhi ya viongozi na wanavijiji walikua wakifanya. Kila kijiji jumla ya hatimiliki za kimila 50 zilipatikana na kufanya hatimiliki 150 kwa vijiji vyote na maeneo kupangwa kwa mujibu wa mahitaji yao kama wananchi.

3.6.2 Mpango wa matumizi ya ardhi kijiji cha Wambingeto na Lugalo wilaya ya Kilolo

Kuanzia tarehe 9-26/11/ 2014 Taasisi iliweza kukamilisha utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kwa vijiji viwili tajwa hapo juu na kufanya vijijii kufikia saba kwa wilaya ya Kilolo kunufaika na mpango huu. Hatua zote sita za upangaji wa matumizi ya ardhi zilifanyika kikamilifu kwa ushirikiano wa watendaji kutoka idara ya ardhi, wananchi na viongozi kutoka kwa vijiji husika. Hatua hizo ni pamoja elimu kuhusiana na matumizi ya ardhi vijijini, sheria na kanuni pamoja na uundwaji wa kamati ya matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji (VLUM) unaofanyika kupitia halmashauri ya kijiji na mkutano mkuu wa kijiji, uundwaji wa kamati ya matumizi ya ardhi ngazi ya wilaya (PLUM) ambao ni wataalamu wa wilaya (kutoka idara mbalimbali za

ardhi, maendeleo, maji, misitu n.k) Hatua ya tatu ni uchukuaji wa taarifa za matumizi ya kijiji husika kwa ujumla unaofanywa na kamati zote mbili. Uandaaji na uwasilishaji wa ramani na PLUM kuwasilisha rasimu ya ramani kwa wananchi kupitia mkutano mkuu wa kijiji. Hatua ya upimaji wa mashamba ya wanavijiji na kuhitimishwa kwa hatua ya uandaaji na usajili wa vyeti vya hati miliki ya kimila kwa wananchi wa kijiji husika.

3.6.3 Utoaji wa hatimiliki za kimila katika wilaya za Kilolo na Mufindi

Kuanzia tarehe 9-18/12/2014 taasisi iliweza kugawa hatimiliki za kimila baada ukamilisho wa matumizi ya ardhi wilaya ya Kilolo katika vijiji saba (7). Vijiji hivyo na idadi ya hatimiliki zilizotolewa ni Kihesamgagao (72), Kidabaga (145), Kiwalamo (105), Kitelewasi (65), Kipaduka (74), Lugalo (190) na Uhambingeto (158). Hatimiliki hizi zilitolewa na Mkurugenzi wa HAKIARDHI mbele ya Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye alikuwa mgeni rasmi, waheshimiwa madiwani, watendaji wa vijiji na kata na wawakilishi kutoka halmashauri ya wilaya na idara ya ardhi. Wanavijiji pamoja na viongozi walishukuru taasisi kwa hatua hii ambayo itapunguza changamoto za ardhi ikiwemo migogoro. Wilaya kupitia Mwenyekiti aliishukuru Taasisi kwani shughuli waliyoifanya ni mchango mkubwa kwa serikali maana ni jukumu lake kuu na aliiomba taasisi pale fursa itakapojitokeza waweze kufanya katika vijiji vingine kwani uhitaji ni mkubwa sana kulinganisha na uwezo wa serikali.

Picha 7: Wananchi wa kijiji cha Kihesamgagao wakipokea vyeti vya hatimiliki za kimila.

SURA YA NNE

MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA HITIMISHO

SURA YA NNE

MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA HITIMISHO

Mafanikio ya jumla kutokana na utekelezaji wa kazi mbalimbali za taasisi

- Kumekuwa na ongezeko kubwa la wananchi ambao wamekuwa wakihitaji kupatiwa msaada wa kisheria kwenye maeneo ya programu na kwenye ofisi za Taasisi. Ongezeko hili linatokana na wananchi wengi kupata msaada wa kisheria ambao uliwasaidia kutatua matatizo yao ya ardhi.

- Machapisho yanayoandaliwa na Taasisi yamekuza uelewa wa wananchi kuhusiana na haki na wajibu wao katika rasilimali ya ardhi. Kukua kwa uelewa kumewasaidia wananchi hawa kusimamia haki zao kikamilifu kwa kushiriki kwenye mikutano na vikao vya maamuzi kuhusu ugawaji wa ardhi kwa matumizi mbalimbali.

- Vipindi vya radio na runinga vimekuwa chachu ya kuibua hamasa ya wananchi nchi nzima kuibua vuguvugu la harakati za kudai haki za ardhi ambazo zimekuwa zikikiukwa kwa makusudi na watendaji wa serikali au wawekezaji pamoja na watumiaji wengine wa ardhi. Vipindi hivi vimekuwa chachu kutokana na kuwafikia wananchi maeneo ambayo Taasisi haifiki moja kwa moja lakini matangazo ya radio na runinga yanafika.

- Uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye baadhi ya vijiji vya wilaya za Mufindi na Kilolo mkoani Iringa umewezesha kwa kiasi kikubwa kulinda haki za ardhi za wanavijiji na hasa

hasa wanawake ambao kwa muda mrefu wamedhulumiwa haki zao kutokana na kukosa uelewa wa kisheria kuhusiana na haki zao katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi. Vilevile msaada wa kisheria umewawezesha viongozi na wananchi kulinda na kutunza mazingira kwenye maeneo yao hasa kwa kutunza vyanzo vya maji na kudhibiti uchomaji wa misitu na mkaa kiholela.

Changamoto za ujumla katika utekelezaji wa kazi za taasisi

- Vikwazo vinavyowekwa na baadhi ya watendaji wa serikali katika utekelezaji wa kazi unakwamisha kupatikana kwa matokeo ya kazi husika kwa wakati uliopangwa.

- Ongezeko la uwekezaji mkubwa katika ardhi na wimbi la uuzaji wa ardhi ni changamoto nyingine kubwa ambayo inakwamisha utekelezaji wa kazi kwa ufasha kutokana na wananchi kuathirika na hali hii kwa kiasi kikubwa kabla ya Taasisi kuanza utekelezaji wa kazi zake.

- Ucheleweshaji wa kupata fedha kwa wakati kutoka kwa wafadhili ni changamoto nyingine ambayo hukwamisha utekelezaji wa kazi kama zilivyopangwa na hivyo kupelekea kazi hizo kutekelezwa katika muda ambao sio sahihi na hivyo kukosa matokeo yaliyokusudiwa.

- Ongezeko la madhara ya mabadiliko ya tabia ya nchi ni changamoto nyingine ambayo inaongeza athari kwenye matumizi na umilikaji wa ardhi kwa wazalishaji wadogowadogo hasa hasa wakulima na wafugaji. Hii inaongeza jukumu jingine katika harakati za kuhakikisha kuwa wazalishaji wadogowadogo wananufaika na rasilimali ardhi.

HITIMISHO

Ripoti hii imeainisha mabadiliko chanya ambayo yamekuwa yakipatikana kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa katika kuhakikisha kuwa utetezi wa haki za ardhi kwa wazalishaji wadogowadogo unahusisha wadau mbalimbali kutoka katika kila sekta kwa lengo la kupata haki stahiki na kwa wakati husika. Jambo kubwa katika ripoti hii ni kuwa uelewa wa wananchi umekuwa mkubwa sana katika utambuzi wa haki zao kuhusiana na rasilimali ardhi, misitu, maji na mazingira kwa ujumla. Ni dhahiri kuwa kadri ambavyo ushirikiano baina ya serikali na taasisi za kiraia unapokuwa wa karibu zaidi na wa kuaminiana ni wakati ambao wananchi watanufaika na sera na sheria nzuri ambazo zitalinda haki zao katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi na rasilimali nyinginezo.